


RONALDO AFURAHIA MSIMU BORA SAUDIA

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Juni 5, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581698
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

## MKOPO TRIL 6.478/-

# Serikali yaanika kilichomo ndani

• **Yasema** Korea Kusini imeshafanya hivyo kwa mataifa mengi...*Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 3

**SAMIA: AJENDA YA NISHATI SAFI IUNGWE MKONO AFRIKA YOTE**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wakuu wa nchi za Afrika...

UKURASA WA 5

DAI LA 'BOOM'

**NCHIMBI AMPA MKENDA WIKI 4 KUMALIZA KILIO**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel...


UKURASA WA 5

**POLISI 3 KIZIMBANI KWA MASHTAKA RUSHWA YA MIL.55/-**

ASKARI watatu wa Jeshi la Polisi Kituo cha Tunduma, wilayani Momba...

**Mfanyakazi Hospitali ya Mnazi Mmoja adaiwa kuuawa na askari JKU**

UKURASA 19




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Operesheni michezo kubahatisha, mfumo malalamiko ya kodi vyaja

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA KUANZIA UGENINI CAF** UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasili Kintex, nje kidogo ya Jiji la Seoul, Jamhuri ya Korea jana, kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa Korea na Afrika. **PICHA: IKULU**

# Operesheni michezo kubahatisha, mfumo malalamiko kodi vyaja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetamka itakamilisha katika mwaka ujao wa fedha mfumo wa kukusanya na kuchakata malalamiko ya walipakodi, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba amesema.

Sambamba na hilo, imesema zitafanyika operesheni maalum nne dhidi ya michezo haramu ya kubahatisha, huku yenyewe ikiendelea kusaka Sh. trilioni 44.19 za kutekeleza mpango na bajeti ya serikali ambazo hivi sasa hainazo.

Waziri Dk. Mwigulu aliyasema hayo bungeni jana alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/25, akiomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 18.287, huku akigusia ajenda nyingine ya 'vita' maalum kukabili ubabaishaji katika ununuzi serikalini.

Alisema vipaumbele vya mafungu ya wizara ni pamoja na kutafuta na kukusanya mapato ya Sh. trilioni 44.19 kati ya maoteo ya Sh. trilioni 49. 35 kwa ajili ya utekelezaji mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Waziri huyo alitaja kipaumbele kingine ni kuimarisha na kusimamia mifumo ya mapato, matumizi na mali za serikali ikiwamo IDRAS, TANCIS, MUSE, NeST, CBMS na GAMIS, pia kuhudumia deni la serikali kwa wakati na kuboresha kanzidata ya kutunza taarifa za deni.

Dk. Mwigulu alisema wizara pia itatoa elimu ya huduma za fedha kwa wananchi kwa lengo la kukuza huduma jumuishi za fedha nchini na kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi pamoja na waratibu wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za umma. Alisema Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kwa mwaka 2024/25 itafanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma kama yalivyoidhinishwa na Bunge mwaka 2023/24.

"Ofisi itafanya ukaguzi wa kiufundi, ufanisi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA, ukaguzi maalum na kiuchunguzi kulingana na mahitaji, kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga na kukarabati ofisi za mikoa na kuzijengea uwezo kamati za kudumu za Bunge za usimamizi na za kisekta ili kuzielewa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kuhusu vipaumbele vya taasisi za wizara kwa mwaka 2024/25, waziri huyo alisema Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatarajia kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya Sh. trilioni 29.42. Kati yake, Sh. trilioni 28.87 ni mapato ya kodi na Sh. bilioni 541.10 ni mapato yasiyo ya kodi. Alisema mamlaka pia itaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti biashara za magendo ili kupunguza mianya ya upotevu wa mapato ya serikali.

Alisema Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu inatarajia kusajili wahasibu na wakaguzi wa hesabu 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama.

Waziri Mwigulu alisema katika mwaka ujao wa fedha watatekeleza operesheni nne za kutokomeza michezo haramu ya kubahatisha, kukusanya mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha ya jumla ya Sh. bilioni 24.89, kuendelea kuelimisha jamii juu ya athari hasi za michezo ya kubahatisha na kusimamia uendeshaji Bahati Nasibu ya Taifa.

Ili kutekeleza majukumu hayo, aliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 18.17 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya wizara hiyo.

Kati ya fedha hizo, Deni la Serikali ni Sh. trilioni 13.132, Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Sh. bilioni 14.276, Tume ya Pamoja ya Fedha Sh. bilioni 6.006, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu Sh. bilioni 3.768, Hazina Sh. trilioni 2.130, Huduma za Mfuko Mkuu Sh. trilioni 2.629, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Sh. bilioni 69.655, Wizara ya Fedha Sh. bilioni 188.486 na NAOT Sh. bilioni 112.729.

***SOMA SEHEMU YA HOTUBA YA WAZIRI MWIGULU Uk. 11-17**

# Serikali yatoa ufafanuzi mkopo Dola bil. 2.5

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu mkopo nafuu wa Dola za Marekani bilioni 2.5 (sawa Sh. trilioni 6.7) uliotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini na kuzua maswali baada ya habari yenye dosari kama ilivyotangazwa na baadhi ya vyombo vya habari vya kimataifa.

Ufafanuzi huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu upotoshaji uliofanywa na vyombo hivyo.

"Korea haijapewa sehemu ya bahari yetu tunachofanya ni kushirikiana nao kupata uzoefu na utaalamu kutoka kwa rafiki zetu hao ili kuboresha shughuli zetu za uvuvi kwa kutumia utaalamu wa hali ya juu na teknolojia mbalimbali," alisema.

Alisema sio Tanzania pekee inayopata mkopo wa aina hiyo na kufafanua kuwa ziko nchi 59 ambazo zimekwishapata mikopo ya aina hiyo kwenye mabara ya Afrika, Asia na Ulaya na haziweki rehani mali zake.

Alisema taarifa hizo zilisambaa jana kwenye mitandao ya kijamii na kwenye mashirika ya habari ya kimataifa yakiwamo baadhi ya magazeti ya Afrika Mashariki na kusababisha taharuki kubwa.

Alisema kwenye ziara hiyo Rais Samia Suluhu Hassan, ameshuhudia utiaji saini wa nyaraka tatu ambazo ni mkataba na nyaraka zingine mbili ni za makubaliano (MoU) na tamko la pamoja baina ya mataifa hayo mawili.

Alisema katika mkataba ambao Rais Samia ameshuhudia utiaji saini wake unahusu mkopo wa Dola za Marekani bilioni 2.5 kwa ajili ya miradi ya miundombinu chini ya mfuko wa ushirikiano wa kiuchumi baina ya Tanzania na Korea (IDCF).

"Mkopo huu kama ulivyoelezwa na Balozi wetu Korea, Togolani Mavura na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, huu ni mkopo wa masharti nafuu na utatolewa ndani ya miaka mitano kuanzia sasa na utaanza kulipwa baada ya miaka 25 kupita kwa hiyo tumepewa unafuu huo," alisema.

"Mkopo huo utalipwa kwa kipindi cha miaka 40 na tunaposema ni mkopo nafuu ni kwa sababu riba ya mkopo huu ni asilimia 0.01 kwa hiyo riba hiyo ni ndogo sana. Serikali haijaweka rehani kitu chochote wala mali yoyote kama ambavyo imepotoshwa kwenye majukwaa mbalimbali," alisema.

Kadhalika, mkopo huo hauna masharti ya kuweka rehani kitu chochote na sio mara ya kwanza kwa Tanzania kupata mkopo wa aina hiyo chini ya mfuko huo IDCF.

Alisema Tanzania imeshapata mkopo wa aina hiyo mara mbili na mara ya kwanza ilipata Dola za Marekani milioni 733 mwaka 2014-2022 na mara ya pili ilipewa mkopo wa Dola za Marekani bilioni moja kwa mwaka 2021-2025.

Baadhi ya miradi mingine iliyotokana na ushirikiano baina ya Tanzania na Korea na mikopo ya aina hiyo iliyotajwa ni ujenzi wa Hospitali ya Mloganzila, uboreshaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Daraja la Tanzanite jijini Dar es Salaam, Daraja la Jakaya Kikwete, Mto Malagalasi na uunganishaji wa Mkoa wa Kigoma kwenye gridi ya taifa ya umeme.

Mingine ni mradi wa majisafi na taka mkoani Iringa, awamu ya kwanza ya mradi wa vitambulisho vya taifa vya NIDA, Bandari ya Uvuvi Bagamoyo, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano na Maonesho Zanzibar.

Kadhalika, mradi wa Hospitali ya Binguni Zanzibar, Chuo cha TEHAMA jijini Dodoma na mradi wa umwagiliaji Zanzibar.

## HABARI KITAIFA

# Samia ataka Afrika kuunga mkono ajenda nishati safi

**Na Salome Kitomari,** KOREA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wakuu wa nchi za Afrika kuunga mkono ajenda ya nishati safi ya kupikia itakayotatua changamoto za kiafya kwa wanawake na kupunguza uharibifu wa mazingira katika kufikia lengo 7(1) la Malengo ya Milenia.

Aidha, ameiomba serikali ya Jamhuri ya Korea ambayo ni taifa la 12 kwa uchumi mkubwa duniani, kuunga mkono ajenda hiyo ili kupunguza matatizo ya uharibifu wa mazingira na kuwaokoa wanawake na wananchi kwa ujumla.

Lengo namba saba la Milenia linazungumzia nishati ya bei nafuu na safi ifikapo 2030 huku Tanzania ikiweka mkakati wa kufikisha nishati safi ya kupikia kwa zaidi ya asilimia 80 ya wanawake ifikapo 2034.

Akizungumza katika mkutano wa wakuu na serikali kati ya Korea na Afrika unaoendelea katika mji wa Goyang, Seoul Korea, uliowaleta pamoja marais 28 na wawakilishi wa wengine 23 barani Afrika kujadili ushirikiano baina ya nchi hiyo na ukanda huo, alisema pamoja na Tanzania kutoa maoni yake kwenye ajenda ya Korea-Afrika, lakini ni muhimu kuwekeza kwenye nishati safi ya kupikia.

Rais Samia ambaye ni kinara wa nishati safi ya kupikia kwa wanawake Afrika, alisema nishati safi itapunguza ukataji miti na magonjwa yatokanayo na hewa chafu na kuwaunguzia wanawake usumbufu.

"Mimi ndiye Rais mwanamke pekee katika chumba hiki (2024 Korea-Afrika Summit), lazima nizungumzie ajenda ambayo ni muhimu kwa mwanamke na kwa ujumla. Nchi yangu (Tanzania) inapenda kusisitiza haja ya kuimarisha ushirikiano ili kuendeleza ajenda ya nishati safi ni sehemu yake na kuongeza uwekezaji katika suluhu za kupikia safi ambako sio tu kwamba hupunguza uzalishaji hewa chafu na kupunguza ukataji miti, lakini pia tunapunguza vifo vinavyohusiana na kupumua na kuwawezesha wanawake kufanya shughuli nyingine za kiuchumi," alisema.



Alisema uwekezaji kwenye nishati safi utaleta suluhisho sehemu nyingi ikiwamo kupunguza hewa chafu, ukataji miti na vifo vitokanazo na njia ya hewa (kupumua) na wanawake kutumia muda kweye shughuli nyingine za uzalishaji.

"Uwekezaji kwenye nishati safi ya kuopikia barani Afrika utatoa fursa za kiuchumi kwa maendeleo ya nchi hizo na ndio maana yeye (Rais Samia) na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Dk. Akinwumi Adesina tunafanya kazi ya kuchangisha fedha kwa ajili ya ajenda hii.

"Hivyo katika suala hili kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba serikali ya Jamhuri ya Korea kuungana nasi katika jambo hili adhimu."

Kuhusu mkutano huo, akitoa maoni yake alisema ni fursa nzuri kwa Afrika kuunda ubia wa kiuchumi wenye nia thabiti katika kukosekana kwa usawa kwenye maendeleo ya kiuchumi ya kijamii kwa nchi hizo.

"Ni matarajio yetu kuwa ubia wa kiuchumi baina ya nchi zetu na Jamhuri ya Korea ni muhimu na mkubwa, tumekusanyika hapa Seoul tukiwa na imani kubwa kwamba mkutano huu unaweka msingi wa kuimarishwa ushirikiano wa kiuchumi na kubadilishana kwa teknolojia na manufaa yake kwa nchi zetu,"alibainisha.

Kwa mujibu wa Rais Samia, inatia moyo kwamba kutakuwa na utaratibu wa kufuatilia uamuzi wa mkutano huu na kuwa na matokeo chanya kutokana na nia iliyoonyeshwa na Korea.

"Na katika muktadha huu, Tanzania inakaribisha dhamira na ahadi za Korea katika kukuza ustawi na ari ya ukuaji wa pamoja. Tunaunga mkono kuweka mifumo ya kukuza uwekezaji wa biashara na ushirikishwaji kwa serikali na sekta binafsi.

"Kwa sasa Tanzania inafanya kazi na Kampuni ya Korea katika uchimbaji wa madini ya kinywe (Graphite). Tunakaribisha ushirikiano zaidi katika uwekezaji kwenye madini ya kimkakati na Watanzania kupata manufaa ya moja kwa moja kutokana na uwekezaji na ustawi wa sekta hiyo," alisema.

Mkutano huo unafanyika miaka 18 tangu Korea ipate hadhi ya kuwa mwangalizi katika Umoja wa Afrika, huku nchi hiyo ikibadilisha uchumi wake kutoka wa chini ukilingana na baadhi ya nchi za Aftrika lakini miaka 70 sasa imepiga hatua kubwa licha ya kuwa na uchumi wa kilimo na raslimali chache.

Mkutano huo unafikia kilele leo kwa kauli ya pamoja ya wakuu hao wa nchi kwa wakati huu ambao Jamhuri ya Korea imeamua kufungua uchumi wake kuelekea Afrika.

Katika kikao cha Rais Samia na Rais wa Jamhuri ya Korea, Yoon Seok-Yeol, walikubaliana ushirikiano katika sekta mbalimbali ikiwamo kwenye madini ya kimkakati ambayo ni Nickel, Lithium na Kinywe yanayopatikana katika maeneo mbalimbali nchini.

Sekta nyingine ni miundombinu, uchumi wa blue kwenye uvuvi na fursa nyinginezo, maendeleo ya gesi asilia, sekta ya ubunifu kwa lengo la kukuza uchumi, kuongeza ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

## HABARI KITAIFA

# Kesi ya wanandoa kujeruhi, ushahidi kuendelea Juni 25

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI wa upande wa mashtaka, Kiran Lalit Ratilal ameshindwa kutoa ushahidi katika kesi ya kujeruhi inayowakabili wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54) kwa kuwa wakili wa utetezi katika kesi hiyo ana shauri lingine Mahakama ya Rufani.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya India wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, Dar es Salaam wanashtakiwa kwa mashtaka manne, likiwamo la kujeruhi, waliyodaiwa kuyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

Kesi hiyo ililetwa juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka. Mashahidi watatu wameshatoa ushahidi wao.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Grace Mwanga alidai kuwa wana shahidi mmoja na walikuwa tayari kuendelea na ushahidi.

Hata hivyo, baada ya kutolewa taarifa hiyo mahakamani huko, upande wa utetezi ulidai ni kweli kesi ipo kwenye hatua ya ushahidi, lakini isivyo bahati, siku ya Ijumaa walipata barua kutoka Mahakama ya Rufani.

Baada ya Mshobozi kudai hayo, Wakili Mwanga alidai kutokana na maombi hayo hawana pingamizi, wakaomba wapangiwe tarehe nyingine ya usikilizwaji ambayo alipendekeza iwe Julai mwaka huu. Hakimu alisema ni mbali sana.

Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 25, 2024 kwa ajili ya usikilizwaji, shahidi Kiran Lalit aliamriwa na mahakama kufika mahakamani siku hiyo kwa ajili ya kutoa ushahidi.

"Wakili wa washtakiwa hayupo, tumeelezwa hapa yupo Mahakama ya Rufani, unatakiwa tarehe tutakayopanga uwapo mahakamani," aliagiza hakimu.



Wakili na mwanaharakati wa haki za binadamu, Maduhu William, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kutekwa kwa mtoto mwenye ualbino mkoani Kagera na kuliomba jeshi la polisi kufanya jitahada ili wahusika wakamatwe. **PICHA: SABATO KASIKA**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
03.06.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya **tarehe 05.06.2024 hadi 11.06.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga**, gari hilo lenye namba za usajili

   **NRB97300 / NRB54202**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 28.0 Upana - mita 5.70 Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: Bandari ya **Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia Barabara ya **Mandela**, Barabara ya **Morogoro** gari litasafiri muda wa mchana **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**







# Binti adaiwa kubakwa kisha kuuawa kikatili

**Na Vitus Audax,** MWANZA

- Wanaodaiwa wapenzi wake wakamatwa

MWILI wa binti mwenye umri wa miaka (17), mkazi wa Nyamanoro, wilayani Ilemela, mkoani Mwanza umekutwa katika uchochoro ukiwa hauna nguo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, alisema jana kuwa mwili huo uligundulika Mei 27 mwaka huu saa 12 asubuhi katika Mtaa wa Nyamanoro Mashariki.

Alisema kuwa baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wananchi, askari wake walifika eneo la tukio na baada ya kukagua mwili huo, mwili wa binti huyo ulikutwa na michubuko mgongoni na kwenye mkono wa kushoto.

Kamanda Mutafungwa alisema mwili huo ulipelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Sekou Toure) ambako uchunguzi wa awali ulibaini kuwa binti huyo aliuawa na mwili ulikutwa na dalili za kuingiliwa kimwili.

"Katika tukio hilo tunawashikilia watu wawili ambao ni Jovin Kamando (26), mkazi wa Kilimahewa jijini pamoja na Kelvini Raymond (27), mkazi wa Kitangiri jijini ambao wote wanasemekana walikuwa na uhusiano wa kimapenzi na binti huyo," alisema Kamanda Mutafungwa.

Kwa umri wa miaka 17 aliokuwa nao binti huyo unamweka katika kundi la watoto. Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2009 inazuia kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtoto.

Vilevile, Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, inaelekeza adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani kwa anayekutwa na hatia ya kubaka mtoto au kifungo cha maisha gerezani kwa wanaobaki wakiwa katika kikundi.

Kamanda Mutafungwa alisema chanzo cha tukio hilo kinasadikiwa kuwa ni wivu wa kimapenzi na uchunguzi unaendelea. Ukikamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria.

Alisema Jeshi la Polisi linaomba wananchi wote wenye taarifa zozote juu ya tukio hilo waziwasilishe ndani ya jeshi hilo huku akitaka wakazi wa mkoa huo kujiepusha na matukio ya mauaji.

Kamanda Mutafungwa pia alithibitisha jeshi hilo kushikilia watu sita kwa tuhuma za kumuua mama yao mzazi, Shija Magelanya (77) wakimtuhumu kuwaroga wajukuu zake na kuwasababishia wendawazimu.

Alisema tukio hilo lilitokea Juni Mosi mwaka huu saa 2:30 usiku katika Kijiji cha Nduwa, Kata ya Kasororo, wilayani Misungwi ambako bibi huyo, akiwa amekaa na wajukuu zake wakila chakula, ghafla walivamiwa na mwanaume aliyekuwa na panga kisha akaanza kumkata maeneo ya kichwani na mabegani na kusababisha kupoteza maisha papohapo.

"Chanzo cha tukio hilo ni imani za kishirikina ambapo watoto wa bibi huyo wamekuwa wanamtuhumu mama yao kuroga wajukuu zake na kuwasababishia wendawazimu na hata vifo ambavyo vimekua havieleweki nyumbani kwao," alisema Kamanda Mutafungwa.

**HABARI KITAIFA**

## Polisi watatu kortini mashtaka ya rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOMBA

ASKARI watatu wa Jeshi la Polisi Kituo cha Tunduma, wilayani Momba, mkoani Songwe wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka ya kuomba na kupokea rushwa Sh. milioni 55 kutoka kwa mfanyabiashara wa vipodozi.

Washtakiwa hao walifikishwa jana katika Mahakama ya Wilaya ya Momba na Maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Songwe na kusomewa mashtaka hayo.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa washtakiwa hao walifukuzwa kazi na jeshi hilo kabla ya kukamatwa na maofisa wa TAKUKURU kwa tuhuma hizo.

Washtakiwa hao ni Koplo Enock Marando (43), Koplo Samson Kalebe (38) na Konstebo Zawadi Malakasuka (39).

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Timoth Lyon, Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe, Simona Mapunda alidai kuwa Machi 7 mwaka huu, katika Mpaka wa Tanzania na Zambia ulioko Mji wa Tunduma, washtakiwa hao walimwomba mfanyabiashara, Halima Abdallah kiasi hicho cha fedha baada ya kumkamata na shehena hiyo ya vipodozi vilivyopigwa marufuku na serikali.

Mapunda alidai kuwa washtakiwa hao, wakiwa ni waajiriwa wa Jeshi la Polisi, waliomba rushwa ya kiasi hicho cha fedha huku wakijua kuwa ni kinyume cha kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria ya Rushwa.

Hakimu Lyon baada ya kusikiliza maelezo ya kesi hiyo ya rushwa namba 15094 ya mwaka 2024 na washtakiwa hao kukana kutenda makosa hayo, aliiahirisha hadi Juni 18 mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikiliza hoja za awali.

Washtakiwa hao walirudishwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana kwa kila mmoja kuwa na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika zenye thamani ya Sh. milioni 22.5 kila mmoja na kuwasilisha bondi ya Sh. milioni 19.

# Anayetuhumiwa kumuua mtoto wa kambo akamatwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro limemkamata Erick Julias (39), mkazi wa Mlimba kwa tuhuma za kumuua, kumtenganisha kichwa na viungo mtoto wake wa kufikia Johnson Ngonyani (6).

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama alisema pia alimnyofoa kichwa na sehemu za siri na kukata viganja vyote viwili.

Kamanda Mkama alisema mtuhumiwa alitenda ukatili huo Juni mosi, mwaka huu majira ya usiku katika kitongoji cha Kigamboni, Kijiji cha Mwembeni, Kata ya Mlimba, Wilaya ya Kilombero.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa baada ya taarifa za raia wema na alipohojiwa na polisi alikiri kufanya mauaji hayo na kutoa ushirikiano wa kuonesha sehemu alikoficha viungo hivyo.

Wakati huo huo, Polisi Mkoa wa Morogoro imemkamata Jovina Mwakiyee (33), mkazi wa Kijiji cha Mang'ula 'A' kwa tuhuma za kula njama na kumuua mume wake wa ndoa.

"Tukio hili limetokea Juni mosi, mwaka huu usiku katika kitongoji cha Gendeni, Kijiji cha Mang'ula A, Wilaya ya Kilombero ambapo mtuhumiwa huyo alikula njama zilizofanikisha kuuawa kwa mume wake huyo Christian Tungaraza (39), ambaye ni mwalimu mkuu shule ya msingi Signal," alisema.

Kamanda Mkama alisema mwalimu huyo akiwa amelala na mtuhumiwa na watoto wao wawili, alivamiwa ndani na kuuawa kwa kupigwa na kitu butu kichwani.

Alisema baada ya mauaji hayo, jeshi la polisi linaendelea na uchunguzi zaidi ili kuwapata watuhumiwa wengine ambao wanatuhumiwa kushirikiana na mwanamke huyo.

Katika tukio lingine la mauaji, polisi imemkamata Hassan Mbwambo (31), mganga wa kienyeji mkazi wa Same mkoani Kilimanjaro, John Matunda (20), dereva wa bodaboda mkazi wa Dumila wilaya ya Kilosa, Boniface Mwendi (31) na Neema Mbwambo (32) mkazi wa Wilaya ya Moshi Vijijini kwa tuhuma za mauaji ya mfanyabiashara wa madini Elly Kimaro (53), mkazi wa jijini Arusha.

Tukio hilo lilitokea Mei 26, majira ya saa mbili usiku na baada ya kufanya mauaji hayo watuhumiwa hao walimnyang'anya Sh. milioni 15.

Akisimulia namna tukio hilo la mauaji lilivyofanyika, Kamanda Mkama alisema mfanyabiashara huyo alisafiri kutoka Arusha hadi Morogoro akiwa na Mbwambo ambaye ni mmoja wa watuhumiwa kwenda Turiani kwa ajili ya kufanya biashara ya madini.

"Baada ya kufika eneo la Turiani mtuhumiwa kwa kushirikiana na mtuhumiwa mwenzake, Samwel Matunda wakiwa na pikipiki walimteka hadi kijiji cha Berega na kumnyang'anya kiasi hicho cha fedha na kumtaka mume wa marehemu kutuma kiasi kingine cha fedha Shilingi milioni tano ili waweze kumuachia," alisema Kamanda Mkama.

Alisema baada ya kupatiwa kiasi hicho cha fedha watuhumiwa hao walimuua na kutelekeza mwili wa mwanamke huyo katika shamba la mbaazi kijiji cha Berega hadi ulipoonekana na wasamaria wema.

Kamanda Mkama aliwataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya wenza wao katika maisha kwa kuwa matukio mengi yanahusishwa na mapenzi, lakini pia yapo yanayohusisha imani za kishirikina, tamaa za kupata mali na fedha pamoja na migogoro ya kifamilia.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda (kulia), akitembelea maonyesho ya kazi bunifu za kikampuni zinazotekelezwa na wanafunzi wa shule 11 za sekondari kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, yaliyoandaliwa na 'Shirika la The Foundation for Tomorrow' kwa kushirikiana na 'JA Africa', wilayani humo jana, kwa lengo la kuwajengea uwezo wanafunzi kubuni na kuyatekeleza mawazo yao ya kumiliki kampuni. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Kilio cha 'boom', Nchimbi ampa siku 27 Mkenda

**Na Romana Mallya,** ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ametoa siku 27 kuanzia jana kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kumaliza tatizo la ucheleweshaji malipo ya fedha za kujikimu (boom) kwa wanafunzi.

Alitoa agizo hilo jana baada ya mwanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Tengeru, Arusha, Digna Nasari, ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Ambureni, kumweleza kuwa ni miezi sita sasa wanachuo hawajapata fedha za kujikimu.

Balozi Nchimbi ambaye amehitimisha ziara yake Arusha na kwenda mkoani Kilimanjaro, alimwelekeza Waziri wa Elimu kutatua tatizo ndani ya mwezi huu.

"Leo ni tarehe 4 Juni, liishe kufikia mwisho wa mwezi huu. Kuna mtu amesema 'mwisho wa mwezi huu ni mbali sana', lakini ninataka niwaambie kama wamesubiri miezi sita, wanaweza kusubiri siku hizo chache.

"Lakini lazima tatizo liishe na liwe na utatuzi wa kudumu, tunapotoka hapa kiongozi wenu atupatie namba ya simu ili tulifuatilie kwa karibu, awe anatupa habari wasije kutuambia wameshalipa kumbe hawajalipa," aliagiza.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, alisema Mwenyekiti wa Kijiji wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Jonas Paranjo, ambaye alikuwa mgombea wa udiwani, ametangaza kurudi CCM.

Katibu wa NEC, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Abdallah Hamid, aliwaomba wananchi kuendelea kuwa na imani na CCM na kuombea viongozi, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, wawe na nguvu na waongeze uzalendo na kufanya kazi ambayo wanaifanya kwa kasi zaidi.

Katibu Mkuu alianza ziara yake mkoani Kilimanjaro jana na baadaye ataihitimisha mkoani wa Tanga baada ya kuzuru pia mikoa ya Singida, Manyara na Arusha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Hongera Daktari Samia kwa kuaminika kimataifa*

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, amepewa shahada ya heshima ya udaktari katika masuala ya usafiri wa anga nchini Korea.

Yote hayo yakimheshimisha kutokana na kuchangia mengi kwenye maendeleo ya Tanzania, Afrika na dunia.

Tunaungana na Watanzania na wengine wote kumtakia Rais mafanikio zaidi yanayogusa mioyo ya wengi ndani na nje ya mipaka.

Mara kwa mara Rais amepata heshima ya shahada ya juu ya udaktari akiheshimiwa kwanza na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kisha cha Zanzibar (SUZA) na karibuni cha Antaria nchini Uturuki. Tunampongeza Rais kwa kuwa anastahili heshima zote, amechangia pakubwa katika juhudi za kimataifa za kuisaidia Afrika kwenye maeneo mengi tukiangalia anachofanya sasa kuhimiza kutumia nishati safi ya kupikia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Katika dhamira hiyo ya kimataifa ya kupunguza uzalishaji wa gesi chafuzi na kulinda mazingira pamoja afya za wanawake na watoto ambao ndiyo wahusika wakuu jikoni, Rais anastahili sifa.

Tunaungana na wengi kutambua na kuheshimu kazi zake kwa kuwa mara nyingi Rais Samia anang'ara kitaifa na kimataifa kwa kusimama na kuonyesha ujasiri na uthubutu katika kubadili mambo yanayowakera wananchi wake.

Ni nguzo iliyobadili upepo uliokwamisha uhuru wa kisiasa na ule wa vyombo vya habari na kumfanya awe mashuhuri zaidi anaposimamia falsafa ya R4.

Tukumbuke falsafa ya R4 anazosimamia ni reconciliation ambayo ni maridhiano au upatanisho, nyingine resilience yaani ustahimilivu, reforms kwa maana ya mageuzi na rebuild akisisitiza kujenga kwa pamoja taifa letu.

Tunampongeza Rais ni dhamira yake ya kutaka taifa lenye maridhiano na umoja wakidugu kwa watu wanaochukuliana (kuheshimiana na kumkubali kila mmoja alivyo) na kusonga mbele.

Tunajua Rais ameleta falsafa ya R4 baada ya miaka saba ya kifungo cha vyama vya upinzani kilichovikataza kufanya lolote kwa kisingizio kwa si muda wa siasa bali ni wakati wa kufanyakazi na kuleta maendeleo.

Kuvifungia vyama vya siasa ni jambo lililoongeza mgawanyiko wa kisiasa na kiitikadi kati ya Watanzania na tofauti hizo zilijionyesha katika mazungumzo ya wananchi ndani ya jamii na katika uchaguzi.

Ikumbukwe kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa 2019 wapinzani walikwamishwa na kuususia lakini katika uchaguzi mkuu wa 2020 CCM ilitwaa majimbo karibu yote 214 ya uchaguzi Tanzania Bara na kuanzisha mjadala mpya wa hatima ya vyama vya upinzani kwenye siasa za uwakilishi bungeni.

Yote hayo Rais ameyaona na kuanzisha maridhiano na uelewano baina ya makundi yote ya kisiasa kuanzia wapinzani, chama tawala na miongoni mwa wanaharakati za demokrasia ndani ya AZAKI.

Tunakubali kuwa anamlinda kila mmoja akianza na wanasiasa, wanawake na mabinti, wazee, wagonjwa ndiyo Tanzania yenye rasilimali watu na viumbe wengine.


Rais amekuwa mlinzi wa wanawake akihimiza ushiriki na ukombozi wa kinamama kuanzia kwenye siasa, nafasi za uongozi na pia kiuchumi kwa kuonyeshwa fursa za maendeleo, mikopo na kuwafuatilia pale wanapokwama.

Ameliongoza taifa na kusimamia kuwarudisha shuleni mabinti walioshindwa kusoma kutokana na shida mbalimbali zilizowakwamisha kuendelea na masomo, akiamini kuwa dunia bila kuwa na elimu maisha yatakwama.

Tunaungana na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Anga cha Korea kusherehekea mafanikio mengi ya Rais Samia na tunampongeza kwa mambo makubwa anayolifanyia taifa na mawazo mema aliyo nayo kwa Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

Muungwana Lazima Nilonge

# *Huyu ni Mchungaji Msigwa 'orijino' wa CHADEMA au...*

**MEI** 29 mwaka huu, CHADEMA, Kanda ya Nyasa, ilifanya uchaguzi wa mwenyekiti wake wagombea wakiwa ni Joseph Mbilinyi 'Sugu' na Mchungaji Peter Msigwa ambaye alikuwa anatetea nafasi hiyo.

Baada ya kupiga kura kulichofanyika Makambako mkoani Njombe, Sugu aliibuka kidedea kwa kupata kura 54 ambazo ni sawa na asilimia 51, huku Mchungaji Msigwa akipata kura 52 sawa na asilimia 49.

Baada ya matokeo kutangazwa, Mchungaji Msigwa anakaririwa na vyombo vya habari akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wagombea wote ambao kura hazikutosha, akimpongeza Sugu kwa ushindi huo.

Alikaririwa akisema hiyo ndiyo demokrasia na nafasi hizo ni za kubadilishana. "Nawashukuru sana viongozi wote wa mkutano huu, kura ndizo zimeamua hivyo mmepata mlichokitaka na nikupongeze Sugu kwa kupata nafasi hiyo, mimi sikuja kwenye chama hiki ili kutaka cheo."

Pia, anaongeza hapo akiahidi kwamba ataendelea kuwa mwanachama na kwamba yeyote anayehitaji ushauri kwa chochote yuko tayari na kwamba wazidi kushirikiana na kuongeza kuwa hahitaji cheo ili kuwa bora.

Hata hivyo, siku chache baada ya kutoa maneno hayo, Mchungaji Msigwa ameibuka upya akipinga matokeo akirusha tuhuma ambazo anadai zilisababisha ashindwe katika uchaguzi huo.

Lakini, kabla ya kuendelea, ninaomba ieleweke kuwa hapa siyo kupinga tuhuma anazotoa Msigwa, kwa sababu yeye alikuwa kwenye eneo la tukio, bali ninachokieleza ni kwa nini anatoa kauli zinazopingana kwa suala moja?

Ina maana Mchungaji Msigwa aliyekaririwa akipongeza na kuahidi kutoa ushirikiano baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa ni mwingine na huyu ambaye sasa anapinga uchaguzi huo ni mtu mwingine?

Hivi baada ya matokeo alishinikizwa kupongeza au kushukuru? Kwa nini sasa abadilike aje na kauli nyingine tofauti na ile ya awali? Au ndiyo kauli ambazo zimekuwa zikisemwa kuwa 'usimwamini mwanasiasa'?

Kwa sasa amekata rufani kupinga matokeo ya uchaguzi uliompa ushindi Sugu, anadai kuwa katika uchaguzi huo kulikuwa na ukiukwaji wa kanuni za katiba katika upigaji kura pamoja na kufanyika kwa fujo ambazo zilichangia kuharibu uchaguzi huo.

Mbali na kukata rufani anasema, kama chama kitashindwa kufanyia kazi barua yake ya kukata rufani, kitashindwa kujitofautisha na CCM katika kuminya demokrasia na haki.

Vilevile, anakishauri chama chake kijitafakari upya na kurudi katika misingi yake ya haki na demokrasia kwa kuheshimu mawazo ya watu wote wakiwamo wanachama, bila kuwapinga na kuwapuuza kwa kuwa kupishana kwa hoja ndio ukomavu wa kisiasa.

Kimsingi ushauri wake ni wa muhimu, lakini swali langu ni kwamba kwa nini alipongeza uchaguzi huo na sasa anageuka na kupinga matokeo? Kwa nini hakupinga wakati matokeo yanatangazwa?

Huyu ni Mchungaji Msigwa mwingine wa CHADEMA au yule yule aliyekubali matokeo na kuahidi kutoa ushirikiano kwa mpinzani wake? Kwa nini abadilike ghafla na kuja kivingine?

Ninadhani ipo haja kwa wanasiasa kujenga mazingira ya kuaminika, kwani utata wa kauli zao umekuwa ukisababisha baadhi ya watu waseme kuwa wanasiasa si wa kuaminika wanabadilika wakati wowote.

Kwa tuhuma anazotoa kwa sasa, maana yake ni kwamba kauli yake ya kwanza ilikuwa si ya kweli na sasa ndio anasema ukweli wa kile kilichotokea katika uchaguzi huo? Binafsi na hata wana CHADEMA wengine ametuacha njia panda.

Ninaamini kwamba wale wote walisikia kauli ya kwanza, watakuwa wameshindwa kuelewa ni kwa nini sasa ameibuka na tuhuma ambazo angezitoa tangu mwanzo badala ya kutoa neno la shukrani.

Kwa hali hiyo nina neno kwa CHADEMA ushauri wangu kumbuke hayo si mazuri kwenye kusherehekea uhuru wa kutoka kifungoni baada ya miaka saba ya vitisho kwa vyama vya upinzani na kuzuiliwa kufanya kazi zenu na serikali ya awamu ya tano.

HABARI KITAIFA

# Vyuo 40 Tanzania kushirikiana na vya China

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO 40 vya elimu ya ufundi stadi vya Tanzania na vyuo vinane kutoka China vimesaini makubaliano ya ushirikiano wa kuendeleza ujuzi na vyuo vya ufundi stadi vya Tanzania.

Makubaliano hayo yalisainiwa jana na wawakilishi wa vyuo hivyo mbele ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Profesa James Mdoe.

Walisaini makubaliano hayo kwenye kongamano lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, Profesa Mdoe alisema kongalamo hilo ni mwendelezo wa ushirikiano katika elimu ya fundi.

Alisema kupitia ushirikiano huo hufanya makongamano mbalimbali yanayovikutanisha vyuo vya ufundi China na Tanzania na hilo ni kongamano la nne.

“Lengo kubwa ni kuendeleza eneo la ufundi stadi kwani wenzetu China wako mbali sana kwenye eneo la ufundi stadi na ndiyo sababu tunapata bidhaa nyingi sana kutoka China na bidhaa zingine zinatengenezwa kwenye viwanda vidogo vidogo sana,” alisema Profesa Mdoe.

Alisema serikali ilitafuta ushirikiano huo ili ione namna ya kupata uzoefu kutoka China wa kuendeleza ufundi stadi ili uzoefu huo utumike kwenye uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa vijana.

Alisema ushirikiano huo umeshaonyesha matunda mengi wapo wafanyakazi wa NACTVET ambao wameshakwenda China kujifunza ufundi stadi na wakati mwingine China inaleta wataalamu wake hapa nchini.

“Katika ushirikiano huu kuna makubaliano baina ya vyuo na vyuo leo tumeshuhudia makubaliano ambayo watabadilishana walimu, wanafunzi kwenda kule kujifunza kwa muda mfupi na hata kubadilishana teknolojia na utafiti mbalimbali kwa hiyo ni ushirikiano wenye manufaa makubwa,” alisema.

Alisema kwenye ushirikiano huo Tanzania ndiyo imekuwa mnufaika mkubwa kutokana na teknolojia yake kuwa iko chini kulinganisha na China ambayo imepiga hatua kubwa. Alisema Tanzania inarasilimali nyingi ambazo bado hazijafanyiwa kazi hivyo wanapokuja wataalamu wa elimu ya ufundi kutoka China wanawafundisha wenzao wa Tanzania namna ya kuzitumia kupata bidhaa.

Alisema Tanzania imekuwa ikitumia fursa ya ushirikiano huo kuwapa mafunzo wakufunzi wa vyuo vya ufundi ili wapate teknolojia ya juu ya kuendeleza vyuo vyake hapa nchini.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe (wa tatu kushoto), akizindua ushirikiano wa vyuo 40 vya Tanzania na vyuo nane vya China wakati wa kutiliana saini mkataba wa ushirikiano, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Dk. Nchimbi ampa kibarua Makonda kero za wananchi

**Na Romana Mallya,** ARUSHA

WANANCHI 350 jijini Arusha wamewasilisha kero mbalimbali mbele ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ambaye amemwagiza Mkuu wa mkoa huo, Paul Makonda, kwenda kuzitatua kwa kupita kata kwa kata.

Alitoa maelekezo hayo juzi jijini hapa wakati wa mkutano wa hadhara ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kuzungukia mikoa mitano kutatua kero za wananchi na kuangalia utelezaji wa ilani.

Balozi Nchimbi alimwagiza Makonda apite kata kwa kata kuzitatua kero za wananchi mkoani humo.

"Tumekubaliana na Mkuu wa mkoa afanye ziara kata kwa kata kwa ajenda ya kero tu. Bahati nzuri tunamwamini Mkuu wa mkoa," alisema.

Naye, Makonda aliahidi kutekeleza agizo hilo ili wananchi waendelee kuwa na furaha ya Chama cha Mapinduzi.

“Tumepokea na tutatekeleza kwa ubunifu mkubwa,” alisema Makonda.

Katika hatua nyingine, Makonda aliomba kupewa miezi sita ya kusafisha mkoa huo kisha ahamishwe kwingine.

Alisema ifikapo Januari mosi, 2025, Arusha itakuwa namba moja kwa kila kitu kwa kuwa wana kila sababu ya kufanikiwa.



“Nakupa tu mfano mdogo Halmashauri ya Jiji la Arusha mwaka 2023/24, walimwomba Rais Samia Suluhu Hassan, zaidi ya Shilingi bilioni saba na amewaletea asilimia 98, cha kusikitisha fedha waliyotumia ni Sh. milioni 500 tu, wana takribani Shilingi bilioni saba hawajatumia,” alisema.

Alisema ni fedha ambazo Rais aliwapa ili wananchi wa Arusha wapate maendeleo, ambapo mapato ya ndani waliyokusanya ni takriban Sh. bilioni 30 na fedha waliyotumia haizidi Shilingi bilioni nne.

“Jumla ya Sh. bilioni 20 huenda zikarudi mpaka mwaka mwingine wa fedha wakati wananchi wanalia hawana maji, kuna watoto wanakaa chini hawana madarasa, kuna maeneo barabara hazipitiki.

“Hili suala si la Rais Samia au CCM niachieni kwenye huu mkoa niwanyooshe mpaka waseme kazi waliyotakiwa kufanya. Takwimu hizi si zangu nimezipata kwa Mkuu wa wilaya, alisema Makonda.

“Nakuhakikishia hakutakuwa na jiwe litakalosalia juu ya jiwe lazima maendeleo yaliyopangwa na ilani ya CCM yafike kwa kila mwananchi Arusha.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



HABARI KITAIFA

# Wafanyabiashara walalamika makali gharama usafirishaji

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYABIASHARA wanaoagiza mizigo kutoka China wamelalamikia kupanda kwa gharama za ushuru wa kusafirishia mizigo hapa nchini kutoka kwa kampuni za usafirishaji.

Wakizungumza na mwandishi wa gazeti hili jana waliomba serikali kushughulikia tatizo linalochochea kupanda kwa gharama hizo kwa kuwa hali ikiendelea hivyo watalazimika kupandisha bei ya bidhaa ili kufidia.

Mfanyabiashara wa nguo za kike, Beatha James, alisema kuwa wiki iliopita alikwenda kuchukua mzigo wake kwa wakala wa usafirishaji na kutozwa Sh. 2700 kwa gauni moja kutoka Sh. 1700 gharama za awali.

Alisema ongezeko hilo linaathiri mapato katika biashara yake kwa kuwa analazimika kuuza bei iliyozoeleka kwa wateja kwa ajili ya kulinda soko lake.

"Kwa sasa hivi ukisema upandishe bei utapoteza wateja kwa sababu kuna wenzako wengi hawajapandisha bei, kwa hiyo inabidi nikubali kuathiri kipato changu kwa sasa wakati nasubiria serikali inatafanya nini," alisema.

Mfanyabiashara wa viatu, Deo Shayo, alisema ametozwa Sh. 2800 kwa kila kiatu kutoka Sh. 2000 jambo litanaloathiri biashara yake kwa kuwa ni vigumu kupandisha bei peke yake kwa sasa.

Aliiomba serikali kukaa pamoja na wasafirishaji ili kuona namna gani wanaweza kupunguza gharama hizo zisiendelee kuwaumiza kwa kuwa hali ikiendelea hivyo watalazimika kupandisha bei.

Mfanyabiashara wa pochi na viatu, Hapiness Shirima alisema amelazimika kutouza mzigo wake wa pochi alioupokea wiki mbili zilizopita akisubiria kama wenzake watapandisha bei auze pamoja nao kufidia gharama za usafiri zilizoongezeka.

Akizungumza katika kituo cha habari Mei 21, mwaka huu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, alikiri kuongezeka kwa gharama hizo na kuahidi kuwa serikali inafanya jitihada kukabiliana na changamoto hiyo.

Alisema wanafanya mikakati mbalimbali ili kukabiliana na changamoto hiyo ikiwamo kuongeza kasi ya kuondoa mizigo bandarini ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza miundombinu ya kusafirisha mizigo toka bandarini.

Alisema kwa kushirikiana wa wadau wa usafirishaji wamekubaliana kutafuta kampuni zitakazoweza kusaidia meli zinazounganisha mizigo inayokuja Tanzania.

Mkurugenzi wa Jumuia ya wafanyabiashara wa Kariakoo (JWK), Martin Mbwana, alisema dalili njema zimeanza kuonekana baada ya kampuni za usafirishaji kuanza kushusha gharama.

Alitoa mfano tangu wiki iliyopita gharama za kusafirisha kontena la futi 40 zilishuka kufikia Dola za Kimarekani 7000 (Sh. milioni 18) toka Dola 9000 (Sh. milioni 20.3).

Alisema baada ya gharama hizo kupanda waliiomba serikali ipunguze gharama ya bima na usafirishaji ili ushuru usiwe mkubwa na kumuumiza mtumiaji wa mwisho.

"Tukaomba angalau bei ya usafirishaji ibaki palepale angalu dola 2500 hado 3000 ambayo tumeizoea ili isiwe kubwa sana tushindwa kukidhi mahitaji ya soko na mlaji wa mwisho akapandishiwa bei," alisema Mbwana.

Kuongezeka kwa gharama za usafirishaji kunaelezwa kusababishwa na meli kutoka bara la Asia kupita njia ndefu ya Afrika Kusini wakikwepa njia fupi ya Suez Canal ambako kunaelezwa kuwa na uharamia.

Sababu nyingine inaelezwa kuwa ni uhaba wa meli ambazo nyingi zinaelekea bara la Ulaya pamoja na uhaba wa kontena za kubeba mizigo.

## Miaka 20 jela kukutwa na nyama ya swala

**Na Judith Julius,** NGARA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Ngara Mkoa wa Kagera, imewahukumu watu wawili kifungo cha miaka 20 jela kila mmoja kwa kosa la uhujumu uchumi.

Washtakiwa hao ni Gabagambe Itwaza (48) na Ijenela Emmanuel (23), wakazi wa kijiji cha Kamli kilichopo wilayani Ngara.

Hakimu Emmanuela Kavalo wa mahakama hiyo akitoa hukumu hiyo, alisema mahakama imeridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri na kubainisha kuwa kila mmoja atatumikia kifungo cha miaka 20.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lawrence Liwanda, alidai washtakiwa hao walikamatwa Mei 22, 2023 ndani ya Hifadhi ya Buligi, Chato iliyopo kwenye eneo la kijiji cha Kamli. Washtakiwa hao walikamatwa wakiwa na nyama pori ya swala yenye thamani ya Sh. 1,070,700.

Liwanda alibainisha kuwa walikamatwa kwa kosa la kuingia ndani ya hifadhi bila kibali na kumdhulumu swala uhai wake.

Katika utetezi wao, washtakiwa hao waliomba kusamehewa kwa maelezo kuwa wanategemewa na familia zao.

Mwendesha mashtaka, Liwanda, aliiomba mahakama itoe adhabu kali kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwao na kwa wengine ambao wanajihusisha na vitendo hivyo.



Katibu Mtendaji Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Lawrence Mafuru, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Kongamano la Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 linalotarajiwa kufanyika katika ukumbi wa Nkurumah Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Jumamosi Juni 8 mwaka huu. Kushoto ni Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Dk. Mursali Milanzi na Makamu Mwenyekiti wa Timu ya Uandishi ya Dira hiyo, Joseph Semboja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ubelgiji yajivunia ushirikiano miaka 40 na Tanzania

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BALOZI wa Ubelgiji nchini Tanzania, Peter Van Acker amesema nchi yake inajivunia kuwa na ushirikiano mzuri na Serikali ya Tanzania kwa miaka 40 katika nyanja ya uchumi, afya, maji na elimu na itaendelea kudumisha diplomasia pamoja na kuunga mkono jitihada za serikali kusimamia uwiano wa jinsia na demokrasia na utawala bora.

Balozi Van Acker amesema mafanikio hayo yanatokana na Umoja wa Vyuo vikuu vya nchini Ubelgiji na Chuo Kikuu Mzumbe(MU), wilayani Mvomero, Mkoa wa Morogoro kuwa na ushirikiano kwa kipindi cha miaka 10 katika utekelezaji wa programu za kitaaluma kwa kufanya utafiti na kuzitatufitia ufumbuzi changamoto zilizopo kwenye jamii, elimu ya ujasiriamali na upatikanaji wa huduma ya majisafi.

Alisema hayo kwenye hafla ya kufunga programu hiyo ya miaka 10 iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Mzumbe iliyowashirikisha viongozi mbalimbali wa serikali na uongozi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Alisema kuwa nchi yake kupitia ushirikiano wa utafiti mbalimbali imesaidia Serikali ya Tanzania katika mipango yake ya kusaidia kwenye nyanja za kiuchumi, afya, maji na elimu kupitia miradi mbalimbali waliofadhili.

"Kukamilika kwa pragramu hii sio mwisho bali ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Mzumbe na Ubelgiji katika masuala ya kitaaluma utaendelea kwa kutoa ufadhili katika kufanya utafiti mbalimbali utakaosaidia jamii kwenye maendeleo yao," alisema.

Akifunga programu hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Adam Malima, alipongeza jitihada zinazofanywa na Ubelgiji katika kusaidia programu hiyo ya kufanya utafiti wa masuala ya kitaaluma na kijamii na kutaka uendelee katika wilaya nyingine za Mkoa wa Morogoro.

Aliutaka uongozi wa Mzumbe kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya demokrasia na utawala bora kwa viongozi wa serikali za mitaa waliopo madarakani na ambao watakachaguliwa katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Alisema kuwa kazi inayofanywa na Chuo Kikuu cha Mzumbe ni kubwa na serikali ina matumaini makubwa na chuo hicho katika kusaidia kutoa maarifa na ujuzi katika masuala ya uongozi kwa watu.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa William Mwegoha, alisema mradi huo unaotekelezwa na umoja wa vyuo vilivyopo Ubelgiji, umekuwa na manufaa makubwa kwa Chuo cha Mzumbe na serikali kwa ujumla.

Alisema moja ya mafanikio hayo ni pamoja na kupanuka kitaaluma kwa wanataaluma 12 kuhitimu shahada za Uzamivu kwa kufanikisha malengo ya kimkakati ya chuo katika masuala ya Tehama kutengeneza mitaala na kuboresha njia ya ufundishaji.

Alitaja maeneo mengine yaliyoleta tija kupitia mradi huo ni kuwa na wataalamu wenye ubobezi kwenye ubunifu katika ufundishaji na tija kwa chuo na jamii kwa ujumla.



## Watoto wa kike 855 wasitiriwa hedhi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

HATIMAYE wadau wa elimu mkoani hapa, wamewakumbuka wanafunzi wa kike 855 wa shule za msingi na sekondari za Wilaya ya Babati, wanaotoka katika mazingira magumu kwa kuwapatia taulo za kike za kutumia wakati wa hedhi.

Kanzidata ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaonyesha kuwa wanafunzi wa kike walio katika mazingira hayo, hukosa masomo kati ya siku tano hadi saba kila mwezi, sawa na siku 60 hadi 70 kwa mwaka wanapokuwa katika hedhi kutokana na kukosa fedha za kununua taulo hizo

huku baadhi yao wakilazimika kutumia kanga na vitambaa kujisitiri.

Meneja Mradi na Elimu kutoka Shirika la STC, Grace Swai, alisema jana kuwa wanafunzi walionufaika wanatokea shule za msingi 29 na tano za sekondari.

"Tumeamua kuwafikia wanafunzi hawa na kuwagawia taulo za kike zinazodumu kwa miezi 18 hadi miaka miwili baada ya kuguswa na hali wanayokutana nayo katika mazingira yao shuleni.

...Sasa sisi wadau kutoka Shirika la So They Can kuanzia mwaka huu tunawasaidia kukabiliana na hali hiyo ili kuepuka pia kupata maradhi yanayotokana na kutumia nguo wakati wa hedhi."

Aliyataja mafanikio ambayo yamepatikana kutokana na kuwapatia taulo hizo ni ongezeko la wasichana kuhudhuria masomo siku zote, kuongezeka kwa ufaulu, kupunguza magonjwa ya kuambukizwa yanayosababishwa na uchafu na kuhudhuria vipindi muda wote.

Vilevile, alisema suala la taulo limepokelewa na wazazi vizuri kwa kuwa linapunguza gharama kwa wale ambao wanatumia fedha kuwanunulia taulo za kike zinazouzwa dukani.

"Wale wazazi waliokuwa wanatumia shilingi 2,000 kila mwezi kwa mwaka, mtoto mmoja alikuwa anatumia shilingi 24,000, sasa fedha hizo zinatumika kuwanunulia vifaa vya shule zikiwemo sare na madaftari," alisema.

Kwa mujibu wa Swai, utoaji wa taulo utakuwa endelevu kwa kuwa wamewajengea uwezo wanawake vinara watano wa kushona taulo hizo.

Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Oimu, Neema John, alisema taulo hizo zimekuwa mkombozi kwao na kuwasaidia kuhudhuria masomo kila siku bila kukosa.

**Aliyataja mafanikio ambayo yamepatikana kutokana na kuwapatia taulo hizo ni ongezeko la wasichana kuhudhuria masomo siku zote, kuongezeka kwa ufaulu, kupunguza magonjwa ya kuambukizwa yanayosababishwa na uchafu na kuhudhuria vipindi muda wote.**

# Polisi: Watoto waliomlawiti mwenzao hawawezi kushtakiwa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

UTATA wa kisheria sakata la mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka mitatu kudaiwa kulawitiwa na watoto wenzake wawili, umezua gumzo jijini hapa baada ya Jeshi la Polisi kuweka wazi waliofanya tukio hilo, nao hawawezi kushtakiwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi, Justine Masejo, watuhumiwa wa tukio hilo hawawezi kukabiliwa na kesi ya jinai kutokana na miaka yao kuwa chini ya umri wa kushtakiwa kwa kosa hilo.

Watuhumiwa wawili wanaokabiliwa na tukio hilo, mmoja ana umri wa miaka mitano na mwingine tisa.

"Ni kweli suala hilo lina vigezo vyote vya kijinai, lakini sasa kesi hiyo haijafikishwa mahakamani kutokana na umri wa watuhumiwa hao kuwa mdogo kushtakiwa kwa kosa la jinai," alisema na kuongeza: " Sasa mtoto wa miaka mitano, huwezi kumshtaki kwa jinai, hilo shauri linashughulikiwa kinamna nyingine, kati ya Jeshi la Polisi na Idara ya Ustawi wa Jamii."

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwahi kunukuliwa mwaka jana, akisema sheria za Tanzania, zinakataza bayana vitendo vinavyokinzana na tamaduni, mila na desturi na zimeweka adhabu mbalimbali kwa makosa ya namna hiyo na yale ya udhalilishaji kwa watoto, ikiwemo ulawiti.

Aliendа mbali zaidi, akisema uwepo wa matukio yanayokinzana na tamaduni, mila na desturi za Kitanzania, umehatarisha uimara na ustawi wa familia na mustakabali wa Taifa kwa ujumla.

Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania, inatamka bayana kuwa vitendo vya mapenzi kinyume na maumbile, iwe kwa faragha au kwa makubaliano ni kosa la jinai.



Mkurugenzi wa Hoteli ya Amazon, Abdallah Meta (kulia), akipata maelezo ya utunzaji mazingira kutoka kwa mtaalamu wa mazingira, Edward Chande, wakati wa maandalizi ya kampeni ya upandaji miti, hotelini hapo, Mtaa wa Michungwani, wilayani Muheza, mkoani Tanga, mwishoni mwa wiki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wataalamu wa Posta wapigwa msasa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATAALAMU wa masuala ya Posta Afrika wametakiwa kutumia vyema maendeleo ya teknolojia kufungua fursa za kiuchumi na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi zao.

Rai hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Zanzibar, Dk. Mzee Suleiman Mndewa wakati akifungua mkutano wa 42 wa Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Afrika na wa vikao vya wataalamu wa masuala ya posta.

Mkutano huo umewashirikisha wataalamu wa nchi hizo wanachama wa PAPU, ikiwa na lengo la kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Dk.Mndewa, alisema nchi hizo ili ziweze kufanikiwa zaidi katika masuala hayo ni wajibu wao kwa pamoja kuhakikisha kila mmoja anashiriki katika uchumi wa kidigitali.

"Kupitia mkutano huu ni wajibu wetu kuhakikisha tunatafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili nchi wanachama ikiwemo miundombinu na teknolojia ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kurahisisha mawasiliano kwa haraka," alisema.

Posta Masta Mkuu, Maharage Chande, alisema mchango wa posta ni kuhakikisha sheria na mambo ya kiutawala yanasaidia kufanya maboresho katika sekta, kusaidia biashara na uchumi katika nchi hizo.

"Sekta ya posta bado ina mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo kwa kuzingatia masuala ya utawala... ipo haja kwa mataifa haya kuzidi kuimarisha shughuli za kibiashara ili kukuza uchumi wa mataifa haya pamoja na ulipaji kodi, " alisema na kuongeza:

"Tunataka kuzungumza kwa karibu na kuangalia namna tutaweza kufanya biashara kwa urahisi kutoka kusini kwenda kaskazini na tunataka kuhakikisha kanuni zinafuatwa katika kufanikisha biashara hiyo."

Alisema Posta kwa sasa wanajitahidi kuhakikisha hawatumii barua kama zamani, hivyo wanakimbizana kupokea teknolojia ili waweze kutimiza malengo yao .

Awali Katibu Mkuu wa PAPU Afrika, Dk. Sifundo Moyo, alisema kuna changamoto ambazo viongozi wa nchi hizo wameanza kuzitafutia ufumbuzi ikiwemo ajenda ya kuendelea kuwasilisha michango kwa kuzingatia mapato kutoka kwa nchi wanachama ili kufikia malengo kwa kutambua umuhimu wa umoja huo wa Posta Afrika.

Mkutano huo wa 42 wa Baraza la Utawala Afrika umewakutanisha wataalamu kutoka mataifa zaidi ya 15 na ufunguzi wa vikao vya wataalamu wa masuala ya posta kwa maendeleo ya mataifa hayo yanayounda umoja huo.





# Majaliwa: Utekelezaji maono ya Magufuli uko pale pale

**Na Daniel Limbe,** CHATO

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema mpango wa Serikali kujenga tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Kitivo cha Sayansi ya Uvuvi uko palepale katika Kijiji cha Kasagara kama yalivyokuwa maono ya Hayati Rais Dk. John Magufuli.

Majaliwa alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Viwanja vya stendi ya zamani ya mabasi Chato mjini wakati akijibu malalamiko ya wananchi hao kuhusu kusuasua kwa ujenzi huo.

Malalamiko hayo pia yaliwahi kuwasilishwa mwaka jana kwa aliyekuwa Katibu wa Itikadi Uenezi na Mafunzo wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, alipofanya ziara yake wilayani hapa kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Majaliwa aliwataka wananchi hao kuendelea kuiamini serikali kuwa miradi yote iliyoanzishwa na Dk. Magufuli wilayani hapa itakamilika kama ilivyokusudiwa.

Alisema ujenzi wa chuo hicho ambao utekelezaji wake unaendelea kijijini hapo ni muhimu kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa ambao idadi kubwa wanaendesha maisha yao kwa kutegemea shughuli za uvuvi Ziwa Victoria.

"Lengo la ujenzi wa chuo hiki ni kutoa fursa kwa wananchi wa ukanda wa ziwa kuongeza maarifa na ujuzi katika shughuli za uvuvi endelevu na tayari ujenzi wake umeanza kule Kasagara," alisema.

Majaliwa alimuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mandia Kihiyo kuhakikisha anaweka haraka taa kwenye barabara zote za mjini Chato ili kudhibiti vitendo vya uhalifu kwa jamii.

Kwa upande mwingine, Majaliwa aliwaonya wanaume wenye tabia ya kufanya ngono na wanafunzi kuwa sheria imeboreshwa dhidi ya watakaothibitika kuwapa mimba wanafunzi na kukatisha masomo yao.

"Karne hii ni aibu kwa wazazi kuendelea kukatisha masomo watoto kwa madai ya kwenda kuchunga ng'ombe, suala hilo halipaswi kuendelea na kama ni shughuli za nyumbani zifanyike siku za mapumziko ili kutoa fursa kwa watoto kuendelea na masomo yao," alisema.

Ziara ya siku mbili ya Waziri Mkuu Geita ilihitimishwa juzi wilayani hapa kwa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa soko kubwa la kisasa katika mwalo wa ufukwe wa Chato kisha kufanya mkutano huo wa hadhara na kuzungumza na wananchi.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti (mwenye suti ya bluu), akiangalia bidhaa za watoa huduma wa sekta ya maziwa nchini, wakati wa kufunga maadhimisho ya 27 ya Wiki ya Maziwa Duniani katika Uwanja wa Furahisha, jijini Mwanza juzi. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Mabaraza yatokomeza ukatili watoto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MABARAZA ya watoto shuleni na dawati la ulinzi na usalama, yametajwa kuwa na mchango mkubwa katika vita ya kutokomeza ukatili dhidi ya watoto uliokuwa umekithiri mkoani Shinyanga.

Hayo yalibainishwa na Mratibu wa Mpango Mkakati wa Serikali wa Kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) wilayani Shinyanga na Aisha Omary wakati akizungumza na Nipashe.

Aisha alisema Serikali wilayani humo kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, wameanza kazi ya kuhuisha mabaraza hayo pamoja na dawati la ulinzi na usalama kwa shule ambazo yalikuwa yamelala kutokana na kuonekana kuleta mwanga katika vita hiyo.

"Kupitia mabaraza haya tunapata taarifa mapema za vitendo hivyo kupitia viongozi wao kwani watoto hawaogopani kupeana taarifa, tofauti na kumwambia mtu mzima akiogopa kupigwa," alisema.

Alisema kupitia mabaraza hayo kutakuwa na sanduku la maoni shuleni, ambapo watoto watakuwa wakiweka ujumbe wao siku zote za wiki ambayo yanachukuliwa na viongozi na kufanyiwa kazi.

Alitoa wito kwa watoto wanapokuwa wakifanyiwe vitendo vya ukatili wasitunze siri bali watoe taarifa kwa viongozi wao wa mabaraza, kijiji, watendaji kata, maofisa maendeleo, wazazi na polisi jamii.

Mwanafunzi Sophia Silas, ambaye alikuwa mwenyekiti wa baraza la watoto katika Shule ya Msingi Ngh'omango, alisema kupitia mabaraza hayo, taarifa fiche ambazo zimekuwa zikifanyiwa kazi kwa wakati na serikali.

**Aisha alisema Serikali wilayani humo kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, wameanza kazi ya kuhuisha mabaraza hayo pamoja na dawati la ulinzi na usalama kwa shule ambazo yalikuwa yamelala kutokana na kuonekana kuleta mwanga katika vita hiyo.**

# 44.2bn/- kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani Ushetu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI inatarajia kutumia Sh. bilioni 44.2 kwa ajili ya kutatua kero ya maji kwa wakazi wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, ikiwa ni mkakati wake wa kumtua ndoo mwanamke kichwani.

Ni baada ya kusaini mkataba wa mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kutoka Manispaa ya Kahama hadi Ushetu.

Mradi huo utatekelezwa ndani ya miezi 22 na makandarasi wawili chini ya usimamizi wa Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba juzi uliofanyika Kijiji cha Ulowa katika halmashauri hiyo ya Ushetu, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji Vijijini, Mhandisi Clement Kivegalo, alisema mradi huo utawanufaisha zaidi ya watu 189,836.

Kivegalo, alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa matangi matatu, bomba kuu la kupeleka maji lenye urefu wa kilomita 76 kutoka Kahama hadi Ushetu Ulowa na vituo 35 vya kuchotea maji. Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema wakazi wa Ushetu walikuwa na kadhia kubwa kupata maji na kupoteza muda mwingi kutafuta maji ambayo si safi wala salama kwa afya zao na wakati mwingine kulazimika kutumia pamoja na wanyama.

Awesu, aliwataka makandarasi hao kuhakikisha wanakamilisha mradi huo kwa wakati kwa mujibu wa mkataba na kuwapa wakazi wa eneo hilo kazi zisizohitaji ujuzi kama sehemu ya kunufaika kabla ya maji kuanza kutoka.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba aliahidi kuhakikisha anasimamia utoaji wa fedha kwa wakati ili wananchi wapate maji haraka.

Nchemba, alisema serikali imedhamiria kumtua ndoo mama kichwani kwa kuhakikisha maeneo yote nchini yenye ukame yanapata maji pasipo kuchelewa ili kufikia azma yake ya kuwafikia wananchi wote kadri inavyopata fedha.

Mkazi wa Ulowa, Magdarena Mabula, alisema mradi huo utakuwa mkombozi kwao na kwa watoto kupata fursa ya kwenda shule badala ya kubaki nyumbani kuwaangalia wadogo zao mama zao wanapokwenda kutafuta maji.

Wiliamu Samwel, alisema imani kwa wake zao imepotea na kutawala vipigo dhidi yao baada ya kuchukua muda mwingi kutafuta maji badala ya kuwahudumia na watoto wao.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA FEDHA

## HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA MHE. DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2024/2025.



MHE. DKT. MWIGULU NCHEMBA (MB)

WAZIRI WA FEDHA



DKT. NATU EL-MAAMRY MWAMBA

KATIBU MKUU - WIZARA YA FEDHA



MHE. HAMAD HASSAN CHANDE (MB)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA



JENIFA CHRISTIAN OMOLO

NAIBU KATIBU MKUU - WIZARA YA FEDHA



ELIJAH MWANDUMBYA

NAIBU KATIBU MKUU - WIZARA YA FEDHA



AMINA KHAMIS SHAABANI

NAIBU KATIBU MKUU - WIZARA YA FEDHA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB,), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25 DODOMA JUNI 2024

**A. UTANGULIZI**

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana hapa kwa mara nyingine kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2023/24 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25.

3. Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuamini mimi na Naibu Waziri Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb,), kumsaidia kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, hususan katika usimamizi wa fedha za umma na uchumi jumla. Tunapenda kumhakikishia kuwa, jukumu la usimamizi wa fedha za umma na uchumi jumla lipo salama na tutaendelea kusimamia kikamilifu ukusanyaji, utafutaji na ugawaji wa rasilimali fedha kwenye miradi mikubwa ya maendeleo pamoja na huduma za jamii ili kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Tunamwombea afya njema, hekima na busara katika kubadilisha fikra, mifumo na mwelekeo wa Taifa letu kwa maendeleo endelevu na jumuishi ya watanzania.

4. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb,), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb,), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa hekima, busara na weledi wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya kikatiba.

5. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa weledi, umahiri na uadilifu. Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama – Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika – Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Ninawaahidi ushirikiano thabiti katika utekelezaji wa majukumu yao ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika katika kuongoza vikao vya Bunge.

6. Mheshimiwa Spika, pia, nawapongeza waheshimiwa wabunge waliopata heshima ya kuteuliwa kushika nafasi mbalimbali serikalini kati ya Juni 2023 na Mei 2024. Wabunge hao ni Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb,), Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jerry William Silaa (Mb,), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi (Mb,), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba (Mb,), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb,), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

7. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Oran Manase Njeza – Mbunge wa Mbeya Vijijini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe – Mbunge wa Kibiti kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, ninawashukuru pamoja na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kupokea, kuchambua, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2024/25. Maoni na ushauri wao umekuwa na tija katika kuboresha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru waheshimiwa wabunge kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika utekelezaji wa majukumu ya wizara na Serikali kwa ujumla. Kwa niaba ya wizara na taasisi zake, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, tutaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi waliotupa dhamana ya kusimamia masuala ya kisera katika Taifa letu.

8. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wabunge na watanzania wote kwa ujumla, kufuatia vifo vya viongozi wetu wastaafu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina. Aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Ahmed Yahya Abdulwakili aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar. Vilevile, nitoe pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na watanzania wote walioondokewa na wapendwa wao pamoja na uharibifu mkubwa wa mali kutokana na majanga mbalimbali ikiwemo maporomoko ya udongo yaliyotokea Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara na mkoani Mbeya; mafuriko yaliyotokea katika wilaya za Kibiti na Rufiji mkoani Pwani; wilaya ya Malinyi, Ulanga, Mlimba na Halmashauri ya Mji Ifakara mkoani Morogoro; jijini Arusha pamoja na maeneo mengine katika mikoa mbalimbali nchini. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

9. Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba nijielekeze kwenye hoja iliyo mbele yetu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni: Muhtasari wa Majukumu ya Wizara; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24; na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25 ikijumuisha vipaumbele vya Wizara na Taasisi zake pamoja na makadirio ya mapato na matumizi.

**2.0 MAJUKUMU YA WIZARA**

10. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 619A la tarehe 30 Agosti 2023, Wizara ya Fedha imekasimiwa majukumu ya kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi; kusimamia miongozo ya usimamizi wa fedha na mali za Serikali; kuratibu upatikanaji wa fedha na kuimarisha uhusiano wa masuala ya fedha kwa taasisi za kikanda na kimataifa; kuandaa na kusimamia miongozo na utekelezaji wa bajeti ya Serikali; kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina; kuendeleza sekta jumuishi ya fedha; kufuatilia na kutathmini programu za kuondoa umaskini; kudhibiti utakasishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi; kusimamia masuala ya pamoja ya fedha kati ya SMT na SMZ; kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi; kusimamia michezo ya kubahatisha; na kutoa mafunzo ya masuala ya fedha, ununuzi, takwimu na mipango.

**3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24**

3.1 Mwenendo wa Matumizi hadi Aprili 2024

11. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 15.87 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 15.31 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 556.38 matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo shilingi trilioni 13.62, ikiwemo huduma ya deni la Serikali shilingi trilioni 10.48 na matumizi ya mishahara shilingi trilioni 1.69. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 482.55 na fedha za nje shilingi bilioni 73.82.

12. Mheshimiwa Spika, Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi liliidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 97.13 kwa mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida shilingi bilioni 87.72 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 9.41. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo shilingi bilioni 70.83 na mishahara shilingi bilioni 16.89. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 8.83 fedha za nje shilingi milioni 583.88.

13. Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zilizopokelewa kwa mafungu nane (8) ya wizara hadi Aprili 2024 ni shilingi trilioni 11.90, sawa na asilimia 75 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, matumizi halisi yalifikia shilingi trilioni 11.27, sawa na asilimia 95 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo kwa idara, vitengo na taasisi yalikuwa shilingi trilioni 2.07, huduma ya deni la Serikali shilingi trilioni 8.48, mishahara shilingi bilioni 334.48 na maendeleo shilingi bilioni 383.68. Vilevile, hadi Aprili 2024, Fungu 045 limepokea jumla ya shilingi bilioni 81.45, sawa na asilimia 84 ya makisio ya mwaka 2023/24. Matumizi halisi yalifikia shilingi bilioni 77.52, sawa na asilimia 95 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo yalikuwa shilingi bilioni 57.54, mishahara shilingi bilioni 15.55 na shilingi bilioni 4.43 zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilipokelewa na kutumika kwa kila fungu ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na.1 – 3.

3.2 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara

3.2.1 Kukusanya na Kutafuta Mapato ya Jumla ya Shilingi Trilioni 39.79

14. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 39.79, kati ya makadirio yote ya Serikali ya kukusanya jumla ya shilingi trilioni 44. 39 kwa mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho, Fungu 21 lilitarajiwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 39.74 ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 26.73, Idara ya Fedha za Nje shilingi trilioni 5.47 na Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali shilingi trilioni 7.54; Fungu 23 lilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 60; na Fungu 50 shilingi milioni 300. Hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 32.49, sawa na ufanisi wa asilimia 82 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya jumla ya shilingi trilioni 21.31, Idara ya Fedha za Nje shilingi trilioni 4.92, Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali shilingi trilioni 6.18 na maduhuli kupitia Fungu 23 shilingi bilioni 79.23 na Fungu 50 shilingi milioni 950.

3.2.2 Kuhudumia Deni la Serikali

15. Mheshimiwa Spika, kupitia Fungu 001, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 10.48 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali pindi linapoiva. Hadi Aprili 2024, wizara imelipa kwa wakati notisi za madai ya deni lililoiva jumla ya shilingi trilioni 8.48, sawa na ufanisi wa asilimia 81 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.63, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.98 na mtaji shilingi trilioni 2.65, na deni la nje ni shilingi trilioni 3.83, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.34 na mtaji shilingi trilioni 2.49.

3.2.3 Kufanya Tafiti, Tathmini na Mapitio ya Kitaalamu Kuhusu Mifumo ya Usimamizi wa Uchumi, Mipango na Bajeti ya Serikali

16. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kufanya tafiti nne (4) kwenye maeneo ya maendeleo ya sekta ya fedha na uchumi jumla ili kuwezesha maamuzi ya kisera. Aidha, wizara ilitarajia kufanya tathmini ya huduma za wizara kwa wadau na mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24 . Hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kukamilisha tafiti mbili (2), sawa na asilimia 50 ya lengo la mwaka. Aidha, wizara imekamilisha tathmini ya huduma za wizara kwa wadau, mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24 pamoja na kuandaa na kusambaza Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

3.2.4 Kuboresha na Kuunganisha Mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma

17. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kuboresho Mfumo wa Uhasibu Serikalini - MUSE; kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti - CBMS; kuunganisha mfumo wa MUSE na mifumo mingine ya usimamizi wa fedha za umma; kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali - GAMIS; kuunganisha Balozi 10 za Tanzania katika mfumo wa MUSE; kuunganisha taasisi mpya na mfumo wa MUSE; na kuzijengea uwezo taasisi katika matumizi ya mifumo ya usimamizi wa fedha za umma.

18. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuboresha mfumo wa CBMS ili kuongeza ufanisi katika udhibiti wa mipango na bajeti ya Serikali, kuunganisha mfumo wa MUSE katika balozi saba (7) za Tanzania katika nchi ya Ufaransa, Austria, Ujerumani, Uturuki, Uingereza, China na Uswisi na kuboresha moduli tano (5) za mfumo wa GAMIS. Aidha, wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa GAMIS kwa taasisi za umma 269. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kuwezesha taasisi za umma 477 kuandaa taarifa za hesabu za fedha kwa kutumia mfumo wa MUSE, kuwajengea uwezo watumiaji wa mfumo wa MUSE katika balozi 17 za Tanzania na kuunganisha mfumo wa MUSE kwenye taasisi za umma 15.

3.2.5 Kujenga Uwezo wa Watumishi katika Usimamizi wa Masuala ya Fedha

19. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kujenga uwezo wa wakaguzi wa ndani katika sekta ya umma ili kuendana na viwango vya kitaaluma vya kimataifa - Certified Internal Auditor (CIA) na Certified Information System Auditor (CISA); kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani katika taasisi za umma kuhusu matumizi ya mfumo wa ukaguzi - Government Internal Audit Management Information System (GIA-MIS); kujenga uwezo wa wakaguzi wa ndani katika maeneo ya ukaguzi wa taarifa za fedha na mchakato wa ukaguzi unaozingatia vihatarishi; kujenga uwezo wa maafisa masuuli na wenyeviti wa kamati za ukaguzi kuhusu mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani katika taasisi za umma; na kuwajengea uwezo waratibu wa usimamizi wa vihatarishi kuhusu mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za umma.

20. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani 64 kuhusu viwango vya kitaaluma vya kimataifa vya ukaguzi wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za umma; kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani 80 kuhusu matumizi ya mfumo wa GIA-MIS; kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani 724 katika ukaguzi wa taarifa za fedha; na kufanya tathmini ya ubora wa ukaguzi kwa taasisi 140. Aidha, katika kipindi hicho, wizara imefanya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani katika halmashauri 22 za mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Manyara. Vilevile, wizara imetoa mafunzo kwa kamati za ukaguzi katika taasisi za umma 17 pamoja na waratibu wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi 51.

21. Mheshimwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kufanya kaguzi maalumu sita (6) ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Maeneo yaliyohusika na kaguzi hizo ni: Mfumo wa usimamizi wa mapato ya VIZA; malimbikizo ya pensheni kwa wastaafu; madai ya mifuko ya hifadhi ya jamii na Shirika la Taifa la Bima – NIC; ruzuku kwa Shirika la Reli la Tanzania na Zambia – TAZARA; na akaunti za mirathi katika mahakama. Kaguzi nyingine za kimkakati zilizofanyika ni Mradi wa Barabara ya Mabasi Yaendayokasi Awamu ya 4 na 5 katika mkoa wa Dar es Salaam na ufanisi wa miradi nane (8) ya kimkakati katika halmashauri sita (6) Tanzania Bara.

3.2.6 Kuboresha Miundombinu ya Ofisi za Wizara na Taasisi zake pamoja na Miundombinu ya Kufundishia na Kujifunzia

22. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa jengo la wizara katika Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma, ofisi za wizara mkoani Geita, ofisi za Soko la Bidhaa Tanzania na kuwezesha uboreshaji wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia Chuo cha Uhasibu Arusha, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika. Hadi Aprili 2024, ujenzi wa jengo la wizara katika mji wa Serikali Mtumba umefikia asilimia 65, jengo la ofisi za wizara mkoani Geita asilimia 64 na usanifu wa jengo la ofisi za Soko la Bidhaa Tanzania umekamilika na mkandarasi wa ujenzi amepatikana. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 12.36 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kujifunzia na kufundishia inayotekelezwa na Chuo cha Uhasibu Arusha, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika.

3.3 Utekelezaji wa Afua Nyingine

3.3.1 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa wa Masuala ya Kikodi

23. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, wizara imehitimisha majadiliano ya mikataba minne (4) ya utozaji kodi mara mbili kati ya Tanzania na nchi washirika. Nchi hizo ni Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Kisultani ya Oman, Jamhuri ya Iran na mkataba wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo hatua za kusainiwa kwa mikataba hiyo zinaendelea. Aidha, mkataba wa utozaji kodi mara mbili kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu umesainiwa na utekelezaji wake utaanza Januari 2025. Manufaa ya kuhitimishwa na kusainiwa kwa mikataba hiyo ni kuondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi husika, kuvutia mitaji kutoka nje, kuongezeka kwa fursa za ajira, kupanua wigo wa fursa za kibiashara na soko la malighafi, bidhaa na huduma zinazozalishwa na wawekezaji wa ndani. Vilevile, hatua iliyofikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 aya ya 46 (b - d).

3.3.2 Elimu ya Huduma za Fedha

24. Mheshimiwa Spika, wizara inaendelea kupokea maoni na mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wadau kuhusu umuhimu wa elimu ya huduma za fedha kwa umma katika kukuza shughuli za kiuchumi na ustawi wa jamii. Kwa mwaka 2023/24, wizara imeanza kutekeleza Mkakati wa Utoaji wa Elimu ya Fedha Vijijini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Fedha kwa Umma ya Mwaka 2021/22-2025/26. Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais –TAMISEMI, na taasisi za usimamizi ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Dhamana pamoja na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeunda timu maalumu ya wataalamu kutoa elimu kwa umma, hususan vijijini kwa utaratibu wa semina, warsha, makongamano, filamu, runinga, redio, mitandao ya kijamii na mafunzo kwa waratibu waliopo katika halmashauri zetu.

25. Mheshimiwa Spika, makundi yaliyopewa kipaumbele katika zoezi letu linaloendelea la elimu ya fedha kwa umma ni wajasiriamali wadogo, wanawake, vijana, watu wenye mahitaji maalumu na waajiriwa kwa kuwa ni makundi yaliyoathirika zaidi na mikopo ijulikanayo kama kausha damu. Maeneo yaliyofikiwa hadi sasa ni halmashauri za mikoa ya Singida, Manyara na Kagera. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, elimu ya fedha kwa wananchi wetu ni zoezi endelevu; hivyo, elimu itaendelea kutolewa na kuboreshwa kulingana na mazingira, mahitaji na maoni ya wadau. Aidha, kwa kuwa sisi wabunge ni sehemu ya jamii, tunaweza kutembelea mtandao wetu wa elimu ya fedha kwa umma kupitia https://www.youtube.com/@MofURT au HAZINA TV kupata elimu ya fedha, na muhimu zaidi kuwa mabalozi wetu wa elimu ya fedha kwa umma.

3.3.3 Uhakiki na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

26. Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Fedha ni ufuatiliaji na uhakiki wa mahitaji na matumizi ya fedha za umma. Hadi Aprili 2024, wizara imefanya uhakiki wa mapendekezo ya fidia ya jumla ya shilingi bilioni 37.79 kwa wananchi walioridhia kuachia maeneo yao kupisha miradi ya maendeleo. Aidha, wizara imefanya uhakiki wa madai ya fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yaliyotwaliwa na Serikali kwa ajili ya upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Kigoma, Ofisi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na maeneo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika mikoa ya Pwani na Arusha. Vilevile, katika kipindi cha rejea, wizara imetoa nyaraka mbili za udhibiti wa bajeti za mafungu ya kisekta ili kukabiliana na msukumo wa mahitaji ya rasilimali fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan mafuriko. Kadhalika, wizara imeandaa kitabu cha bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 Toleo la Wananchi, na kuandaa taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Serikali kila robo mwaka na kuweka kwenye tovuti ya wizara ili kuongeza uwazi.

3.3.4 Uendelezaji wa Soko la Ndani la Fedha

27. Mheshimiwa Spika, kufuatia mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya fedha, wizara imeendelea kuandaa na kutekeleza miongozo mbalimbali ili kuendeleza soko la ndani la fedha. Kwa mwaka 2023/24, wizara imefanikiwa kuratibu na kuweka sokoni hatifungani ya kijani ya shilingi bilioni 53.12, ikiwa ni hatifungani ya kijani ya kwanza kutolewa na taasisi za umma hapa nchini. Hatua hiyo imefikiwa, ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa njia mbadala. Napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwarobaini wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika taasisi, mashirika na mamlaka za serikali za mitaa umepatikana. Aidha, Wizara ya Fedha iko tayari kushirikiana na taasisi na mashirika ya umma, manispaa pamoja na halmashauri zetu kuandaa nyaraka za matarajio kutafuta fedha kupitia dirisha hili kutekeleza miradi ya kipaumbele bila kutegemea bajeti kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

3.3.5 Maboresho ya Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Kitaasisi

28. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, wizara iliendelea kufanya mapitio na kuboresha miundo ya kitaasisi ili kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu yake. Hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuanzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Ofisi ya Akaunti ya Changamoto za Milenia pamoja na kuzindua na kuwezesha Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi kuanza kutoa huduma. Lengo la kuanzisha taasisi hizo ni kuimarisha na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mipango ya Serikali pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, hususan kuondoa au kupunguza vikwazo vya kibiashara na malalamiko ya walipakodi. Aidha, wizara imefanikiwa kukamilisha mchakato wa kuchagua eneo la ushirikiano na Shirika la Changamoto za Milenia la Marekani - MCC ambapo pamoja na mambo mengine, msaada utakaotolewa na shirika hilo utatumika kutekeleza programu za maendeleo zinazolenga kupunguza au kuondoa vikwazo vya kibiashara.

3.3.6 Uandaaji wa Miongozo ya Kisera na Kisheria

29. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuandaa miongozo mbalimbali ya kisera, kisheria na kitaalamu ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; kuhuisha Mpango Mkakati wa Wizara kuendana na mabadiliko ya muundo na mgawanyo wa majukumu ya Serikali; kutunga upya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 pamoja na kanuni zake; kuhuisha Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani; na kuandaa Mkakati wa Muda wa Kati wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani (2024/2025 – 2026/2027).

3.3.7 Usimamizi wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi

30. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imetoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu ili kuziwezesha Mamlaka za Serikali kuandaa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia. Ushauri na mafunzo ya kitaalamu yametolewa kwa Wakala wa Barabara Tanzania katika kuandaa nyaraka za mradi wa barabara ya haraka kutoka Kibaha hadi Morogoro (kilomita 205) ambapo hatua za ununuzi wa mbia zinaendelea kwa sehemu ya Kibaha - Mlandizi - Chalinze (kilomita 78.9) na Wakala wa Mabasi Yaendayokasi kuhusu ununuzi wa mbia wa uendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayokasi jijini Dar es Salaam. Aidha, mashauriano yanaendelea kuhusu upanuzi na ujenzi wa barabara ya haraka kati ya Morogoro na Dodoma kwa utaratibu wa ubia.

3.3.8 Usimamizi wa Mali za Umma

31. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, jumla ya taasisi za umma 334 zimewezeshwa kuandaa, kuhuisha na kuweka kumbukumbu ya mali zenye thamani ya shilingi trilioni 13.66 katika mfumo wa GAMIS. Aidha, katika kipindi hicho, wizara imetoa vibali 123 vya kuondosha mali chakavu na kuwezesha minada 100 katika taasisi za umma ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.6 zilikusanywa katika minada hiyo. Vilevile, wizara imefanya uhakiki wa mali katika vituo 388 vya Serikali ambapo taarifa zimeandaliwa na mapendekezo kuwasilishwa kwa maafisa

masuuli kwa hatua stahiki.

3.3.9 Huduma za Mafao ya Kustaafu, Pensheni na Mirathi

32. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kusimika Mfumo wa Malipo ya Pensheni - TPPS kwenye taasisi tatu (3) na kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo kwa watumiaji 100. Aidha, wizara imeendelea kulipa kwa wakati mafao ya wastaafu wanaolipwa na Hazina kila mwezi na kuwasilisha stahiki ya michango ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Vilevile, timu ya wataalamu iko mbioni kukamilisha tathmini kuhusu mfumo endelevu wa usimamizi na uboreshaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina.

3.3.10 Udhibiti wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi

33. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu; Kanuni za Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu za mwaka 2023; Amri ya Uteuzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Utakasishaji Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi; na kuanzisha Mfumo wa Taifa wa Takwimu za Udhibiti Utakasishaji Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi.

3.3.11 Usimamizi wa Masuala ya Pamoja ya Fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar

34. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, wizara imekamilisha stadi kuhusu kodi ya zuio katika kampuni na mashirika ya mawasiliano ya simu, benki za biashara na bima zilizosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya biashara katika pande mbili za Muungano. Aidha, uchambuzi wa takwimu kuhusu mwenendo wa mapato na matumizi ya Muungano kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi 2023/24 umekamilika.

3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Taasisi

35. Mheshimiwa Spika, wizara inatekeleza baadhi ya majukumu yake kupitia taasisi ikijumuisha taasisi za elimu; bodi za kitaalamu na kitaaluma; taasisi za benki na fedha; taasisi za usimamizi wa kodi, ununuzi na ugavi na michezo ya kubahatisha; uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi; na takwimu.

3.4.1 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu

36. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, taasisi tano (5) za mafunzo na elimu ya juu zilitarajia kudahili jumla ya wanafunzi 76,272, ikijumuisha ngazi ya astashahada 13,100, stashahada 17,607, shahada 42,337 na shahada ya uzamili 3,228; kuendeleza wahadhiri 210 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili (57) na uzamivu (153); kufanya tafiti 79; na kutoa huduma elekezi 786. Hadi Aprili 2024, taasisi hizo zilidahili jumla ya wanafunzi 75,712, sawa na asilimia 99.3 ya lengo ikijumuisha ngazi ya astashahada 13,778, stashahada 14,654, shahada 42,030 na shahada ya uzamili 5,250. Aidha, jumla ya wahadhiri 180 wamewezeshwa kujiendeleza kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili (44) na uzamivu (136). Vilevile, taasisi zilifanya jumla ya tafiti 48, sawa na asilimia 60.8 ya lengo na kutoa huduma elekezi 142, sawa na asilimia 18.1 ya lengo la mwaka.

3.4.2 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha

37. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilipanga kusajili wahasibu na wakaguzi 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kufanya mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi kwa wahasibu na wakaguzi 12,000; kutoa ushauri wa kiufundi kwa taasisi na kampuni 10 kuhusu matumizi ya viwango vya kitaifa na kimataifa katika uandaaji wa hesabu na ukaguzi; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 75; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 65 za ukaguzi; kufanya mapitio ya mtaala wa uhasibu nchini na kufanya mapitio ya vitabu vya rejea kwa wanafunzi kwa masomo 12; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 12,500; na kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa wahitimu 150.

38. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Bodi imesajili wanachama 2,237, sawa na asilimia 745 ya lengo la mwaka katika ngazi mbalimbali za uhasibu na ukaguzi; imetoa mafunzo kuhusu uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi kwa wahasibu na wakaguzi 11,184, sawa na asilimia 93 ya lengo; imetoa ushauri wa kiufundi kwa taasisi na kampuni tisa (9) kuhusu matumizi ya viwango mbalimbali katika uandaaji wa hesabu na ukaguzi, sawa na asilimia 90 ya lengo; imefanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa hesabu kwa taasisi na kampuni 68, sawa na asilimia 91 ya lengo; na imefanya ukaguzi wa ubora kwa kampuni 52 za ukaguzi, sawa na asilimia 80 ya lengo. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kufanya mapitio ya mtaala wa uhasibu nchini na vitabu vya rejea kwa masomo 12, sawa na asilimia 100 ya lengo; na kusajili watahiniwa 7,238 ambapo 6,711 walifanya mitihani Novemba 2023. Aidha, Bodi iliendesha mitihani kwa watahiniwa 1,451 wenye taaluma za kimataifa. Vilevile, watahiniwa 137 walisajiliwa katika kozi ya diploma ya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma.

39. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ilipanga kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi, kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000. Hadi Aprili 2024, Bodi imesajili watalaamu 1,697 wa ununuzi na ugavi, sawa na ufanisi wa asilimia 48; na kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa watalaamu 2,749, sawa na asilimia 42. Aidha, Bodi imeendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 976, sawa na asilimia 24. Sababu za kutofikia malengo ni hofu ya mabadiliko ya mitaala ya wataalamu wa ununuzi na ugavi yaliyofanywa na Bodi mwaka 2023; na baadhi ya waajiri kutotenga fedha za mafunzo endelevu ya kitaaluma katika bajeti zao kwa wataalamu wa ununuzi na ugavi.

3.4.3 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 26.7; kuendelea kuimarisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato; kuendelea kutoa elimu ya kodi; na kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato. Aidha, Bodi ya Rufani za Kodi, Baraza la Rufani za Kodi na Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi zilitarajia kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri, malalamiko na taarifa za kodi kutoka kwa walipakodi na wadau wa kodi pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma za usuluhishi wa masuala ya kodi.

41. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya jumla ya shilingi trilioni 21.3, sawa na ufanisi wa asilimia 96.9 ya lengo la Julai 2023 hadi Aprili 2024 na asilimia 79.8 ya lengo la mwaka. Aidha, katika kuimarisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato, Mamlaka imeanza ujenzi wa mfumo wa usimamizi wa kodi za ndani - IDRAS ambao ni mahsusi kwa usajili, ukadiriaji, ukusanyaji wa kodi na ufuatiliaji wa walipakodi.

42. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kutekeleza mradi wa kuunganisha mifumo ya ndani na taasisi nyingine za serikali ikiwemo mfumo wa kuzalisha vitambulisho vya Taifa - NIDA na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA na kuboresha moduli ya lango la huduma kwa mlipakodi na moduli ya uwasilishaji wa ritani za kieletroniki kwa mapato ya ndani. Hatua zilizochukuliwa kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato ni pamoja na: kuanzisha divisheni mpya ya walipakodi wa kati na wadogo chini ya Idara ya Kodi za Ndani; kuimarisha mifumo ya kubadilishana taarifa na wadau wa ndani na nje ya nchi; kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya vitendo vinavyoashiria ukwepaji kodi; na kuendelea kuhamasisha wananchi kuhusu masuala ya kodi, hususan umuhimu wa kudai na kutoa risiti za kielektroniki - EFD na matumizi na uhakiki wa stempu za kielektroniki - ETS. Aidha, Mamlaka imetoa elimu ya kodi kwa walipakodi kupitia njia mbalimbali ikiwemo semina, vipindi vya redio na televisheni, matangazo ya kodi, mikutano ya wadau wa kodi, kampeni, mitandao ya kijamii na vipeperushi.

43. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Bodi ya Rufani za Kodi imepokea mashauri ya kodi 437 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 3,456.5 na imesikiliza na kutolea uamuzi mashauri 388 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 2,780.1 na dola za Marekani 439,281. Aidha, Baraza la Rufani za Kodi limesajili jumla ya mashauri 112 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 2,790 ambapo mashauri 64 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 137.9 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi na mashauri 56 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 2,510 yako katika hatua mbalimbali za usikilizaji na kutolewa maamuzi. Vilevile, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi imepokea malalamiko 40, imesuluhisha malalamiko 22 na malalamiko 18 yapo katika hatua mbalimbali za usuluhishi. Kadhalika, Taasisi imeanzisha mfumo wa kupokea malalamiko kwa njia ya simu (call center) ambapo mlalamikaji au mtoa taarifa anaweza kuwasilisha malalamiko kwa kupiga simu ya bure namba 0800111022. Jitihada hizo zimewezesha ongezeko la mwamko wa wananchi na walipakodi kuwasilisha malalamiko yao kwa uhuru na uwazi.

44. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha walipakodi wanakuwa na uelewa na kunufaika na huduma zinazotolewa, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi imeendelea kujitangaza kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja na kufanya vikao na wahariri wa vyombo vya habari na vikundi vya wafanyabiashara katika Mkoa wa Dar es Salaam kuhusu uwepo wa ofisi, majukumu yake na namna ya kuwasilisha malalamiko. Aidha, taasisi imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya umoja wa wafanyabiashara katika mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Lindi na Dar es Salaam kwa lengo la kutoa elimu ya usuluhishi wa masuala ya kodi.

3.4.4 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha

45. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilipanga kutoa leseni 11,880 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo 2,273 ni leseni mpya na leseni 9,607 ni za kuhuisha, kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 101 na kusimamia mchakato wa uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa. Hadi Aprili 2024, Bodi imetoa jumla ya leseni 9,805, sawa na ufanisi wa asilimia 82 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, leseni 6,261 zimehuishwa na 3,544 ni leseni mpya. Aidha, Bodi imekagua jumla ya waendeshaji 87 wa michezo ya kubahatisha, sawa na asilimia 86 ya lengo la mwaka. Vilevile, Bodi imeteua kampuni ya kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa na tayari imesaini mkataba wa uendeshaji kwa mujibu wa sheria ya michezo ya kubahatisha.

3.4.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

46. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kuanzisha bidhaa mpya za masoko ya mitaji; kufanya mapitio ya kanuni na miongozo ya utoaji wa bidhaa katika masoko ya mitaji; na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji na bidhaa. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania lilipanga kuendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa soko wa kielektroniki ili kuongeza idadi ya bidhaa zinazouzwa na kununuliwa kupitia mfumo huo.

47. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imewezesha uanzishaji wa bidhaa mpya na bunifu kwenye masoko ya mitaji ikiwemo hatifungani ya kijani na hatifungani yenye mguso na matokeo chanya kwa jamii; hatifungani yenye mguso wa jinsia; na hatifungani zinazokidhi misingi ya Shariah (Sukuk Bonds). Aidha, Mamlaka imewezesha kutolewa kwa hatifungani ya kwanza Afrika yenye ubunifu unaojumuisha vipengele vinavyogusa taasisi za umma, maboresho ya miundombinu ya maji, utunzaji wa mazingira na miradi yenye uwezo wa kujiendesha kibiashara - Subnational Water Infrastructure Green Revenue Bond iliyotolewa na Mamlaka ya Maji, Tanga. Vilevile, Mamlaka imeandaa Mwongozo wa Kuendesha na Kusimamia Bidhaa za Mitajihalaiki pamoja na Mwongozo ya Utoaji wa Hatifungani Zinazokidhi Misingi ya Shariah. Miongozo hiyo imeidhinishwa na imechapishwa kwenye Gazeti la Serikali kwa matumizi ya umma.

48. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Soko la Bidhaa Tanzania limeendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa soko wa kielektroniki ili kuongeza idadi ya bidhaa zinazouzwa na kununuliwa kupitia mfumo huo. Uhamasishaji umefanyika sambamba na kufanya mauzo ya bidhaa mbalimbali ikiwemo ufuta, kahawa, choroko, mbaazi, chai na kakao. Aidha, mnada wa kwanza wa zao la chai ulifanyika Novemba 2023.

3.4.6 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

49. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Benki Kuu ya Tanzania ilipanga kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi - M3 kwa kiwango



kisichopungua asilimia 10 ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi; kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi; kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4). Aidha, kutokana na mabadiliko ya mifumo ya usimamizi wa uchumi, Benki Kuu ya Tanzania ilianza kutumia mfumo mpya unaotumia riba ya benki kuu ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sera ya fedha, usimamizi wa sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Aidha, utaratibu wa kutumia riba ya benki kuu katika utekelezaji wa sera ya fedha, sekta ya fedha na uchumi jumla unaenda sambamba na mabadiliko ya mfumo wa utoaji taarifa kwa umma.

50. Mheshimiwa Spika, licha ya kukabiliwa na changamoto ya mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia, ukwasi katika uchumi ulitosheleza mahitaji ya shughuli za uzalishaji ambapo ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi - M3 ulikua kwa wastani wa asilimia 15.5 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.1. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 19.2 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 ikilinganishwa na malengo ya ukuaji wa asilimia 16.4. Vilevile, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.5 Desemba 2023 ikilinganishwa na dola bilioni 5.4 Juni 2023, kiwango kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.5, ikiwa ndani ya lengo la nchi la wastani wa miezi 4.

51. Mheshimiwa Spika, sekta ya fedha imeendelea kuwa imara, na vihatarishi kupungua kutokana na matarajio ya uchumi wa dunia kuendelea kuimarika. Sekta ya kibenki ambayo ni sehemu kubwa ya sekta ya fedha imeendelea kuwa imara, yenye kutengeneza faida, ukwasi na mtaji wa kutosha. Ubora wa rasilimali uliendelea kuongezeka, ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 4.3 Desemba 2023 kutoka asilimia 5.5 Juni 2023. Hali hiyo inaashiria kuendelea kupungua kwa vihatarishi katika utoaji wa mikopo kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi pamoja na hatua za kisera na kiusimamizi zinazoendelea kuchukuliwa na benki kuu ili kupunguza mikopo chechefu.

52. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sera ya fedha katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 umewezesha riba ya mikopo ya siku saba (7) katika soko la jumla la fedha baina ya benki kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3.5 hadi 7.5. Wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 17 ambapo sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa kwenye shughuli za kilimo, uchimbaji wa madini, usafirishaji na uzalishaji viwandani. Sekta ndogo ya benki imeendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha, huku ikiendelea kutengeneza faida na uwiano wa mikopo chechefu kuendelea kuwa chini ya asilimia 5 ya mikopo yote.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 45.10, kukuza faida ya benki kabla ya kodi ya shilingi bilioni 18.50, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 120, thamani ya mali za Benki kufikia shilingi bilioni 562.70 na kufuatilia urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wateja shilingi bilioni 62. Hadi Desemba 2023, Benki ilikusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 41.56, sawa na asilimia 92.15 ya lengo na kutengeneza faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 18.79, sawa na asilimia 107.9 ya lengo. Aidha, Benki ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 161.60, sawa na asilimia 134.67 ya lengo na thamani ya mali ilifikia shilingi bilioni 606.94, sawa na asilimia 107.86 ya lengo. Vilevile, Benki ilifuatilia urejeshaji wa mikopo ya shilingi bilioni 92.0, sawa na ufanisi wa asilimia 148.4 ya lengo.

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023, Benki ya Maendeleo TIB ilipanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 11.62 kwa miradi ya maendeleo kwenye sekta ya maji, nishati na uongezaji thamani mazao ya kilimo; kukusanya shilingi bilioni 41.69 kama marejesho ya mikopo kutoka kwa wateja; na kukusanya shilingi bilioni 7.39 ikiwa ni marejesho ya mikopo iliyoshindikana na kuondolewa kwenye mizania ya benki. Hadi Desemba 2023, benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 9.74, sawa na asilimia 83.82 ya lengo. Aidha, Benki ilipokea marejesho ya mikopo ya shilingi bilioni 42.63, sawa na asilimia 102.30 ya lengo. Vilevile, benki ilikusanya shilingi bilioni 6.51 kutoka kwa wateja kama marejesho ya mikopo iliyoshindikana na kuondolewa kwenye mizania ya benki, sawa na ufanisi wa asilimia 88.09 ya lengo.

55. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023, Benki ya Biashara Tanzania ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 184.2; kukuza faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 12.4; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 904; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,121; kukuza mali za benki kufikia shilingi bilioni 1,446; kukuza mtaji kufikia shilingi bilioni 123.8; na kuunda mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo. Hadi Desemba 2023, mapato ya benki yalifikia shilingi bilioni 192.1, sawa na asilimia 104.3 ya lengo; mikopo iliyotolewa ilifikia shilingi bilioni 911.2, sawa na asilimia 100.8; amana zilifikia shilingi bilioni 1,120.7, sawa na asilimia 99.9 ya lengo; mtaji wa benki ulifikia shilingi bilioni 118.9, sawa na asilimia 96 ya lengo; na benki ilikuza mali kufikia shilingi bilioni 1,389.3, sawa na asilimia 96.1 ya lengo. Aidha, benki ilipata hasara ya shilingi bilioni 44.4 kabla ya kodi kutokana na kufutwa kwa mali chechefu iliyorithiwa ya shilingi bilioni 54.4 kutokana na kuunganishwa na benki nyingine tatu (3). Vilevile, mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo unaendelea kusimikwa na kufungamanishwa na mifumo mingine ya benki.

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF ulipanga kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi bilioni 44.8 kwa wajasiriamali 38,000; urejeshaji wa mikopo usipungue asilimia 95; na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa au wanufaika 5,500. Hadi Desemba 2023, Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 49.78, sawa na ufanisi wa asilimia 111 ya lengo kwa wajasiriamali wadogo 37,024, sawa na ufanisi wa asilimia 97 ya lengo la mwaka. Aidha, kiwango cha urejeshaji wa mikopo kilifikia asilimia 95.87 dhidi ya lengo la asilimia 95 kwa mwaka 2023. Vilevile, Mfuko umetoa elimu kwa wadau 2,705, sawa na asilimia 49.1 ya lengo la mwaka. Sababu ya kutofikia lengo la elimu ni kutokana na Mfuko kusitisha utoaji wa mikopo ya vikundi ili kufanya mapitio ya mfumo wa usimamizi wa mikopo kwa vikundi.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS ilipanga kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15; kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5; na kuhamasisha taasisi za Serikali, mifuko ya hifadhi za jamii, mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS. Hadi Aprili 2024, rasilimali za mifuko ziliongezeka hadi shilingi bilioni 2,012.8 kutoka shilingi bilioni 1,535.8 Juni 30, 2023, sawa na ongezeko la asilimia 31.1; na idadi ya wawekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka kwa asilimia 19.2. Sababu za kuvuka malengo ya 2023/24 ni kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu faida ya uwekezaji wa pamoja; matumizi ya teknolojia katika utoaji huduma na ongezeko la mawakala waliosajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilipanga kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 32; kufanya ukaguzi wa kampuni za bima; kuandaa mwongozo wa bima za kilimo; kuhamasisha wadau wa bima kuandaa bidhaa za sekta ya kilimo; na kupokea na kushughulikia malalamiko ya wateja wa bima kwa wakati. Aidha, Shirika la Bima la Taifa lilipanga kukamilisha taratibu za kupata ithibati ya cheti cha ubora cha utoaji huduma kwa wateja (ISO 9001:2015); kuongeza wateja wapya 116 wa bidhaa za taasisi; na kubuni bidhaa tatu (3) mpya zitakazokidhi mahitaji ya soko.

59. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imekamilisha uchambuzi wa mikataba 344 ya bima mtawanyo kwa kampuni 29, sawa na asilimia 90.6 ya lengo; imefanya ukaguzi kwa wadau wa bima 259; kuandaa Mwongozo wa Bima za Kilimo ; na kampuni 14 za bima zimeanzisha Konsotia ya Kilimo - Tanzania Agriculture Insurance Consortium (TAIC) iliyozinduliwa Julai 01, 2023. Aidha, Mamlaka imepokea na kushughulikia malalamiko 288 ya wateja wa bima. Vilevile, Shirika la Bima la Taifa limefanikiwa kupata ithibati ya cheti cha ubora cha ISO 9001 :2015 pamoja na cheti cha ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania ; na kuandikisha wateja wapya 222, sawa na ufanisi wa asilimia 191.4.

3.4.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

60. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kusambaza matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022; kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za sensa; kuendelea kuandaa taarifa za sensa za kisekta kulingana na ratiba; na kufanya tafiti za kitaalamu kuhusu watu wenye uwezo wa kufanya kazi, mapato na matumizi ya kaya binafsi, ajira, mapato na ustawi wa watoto katika jamii.

61. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2024, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kusambaza matokeo ya Sensa kwa kutumia teknolojia ikiwemo tovuti, kanzidata na programu tumizi kupitia simu za kiganjani kwa lengo la kuwafikia wadau wengi iwezekanavyo. Aidha, uchambuzi wa kina, kuandaa kanzidata ya viashiria vya watu wenye ulemavu, utoaji wa elimu na mafunzo kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 umeendelea kufanyika. Uchambuzi unaoendelea kwa sasa ni takwimu za ndoa na uzazi, elimu, hali ya umaskini kwa kutumia viashiria visivyotumia fedha - non-monetary items na makadirio ya idadi ya watu kuanzia mwaka 2023 hadi mwaka 2063. Vilevile, kazi ya uchambuzi wa viashiria vilivyoainishwa katika dodoso la sensa imekamilika kwa asilimia 80 kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Uchambuzi wa Matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022 na ule wa Umoja wa Mataifa. Kadhalika, utoaji wa mafunzo kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 umefanyika kwa asasi za kiraia kupitia vyama vinavyowaunganisha, viongozi wa kimila na mabalozi wa Tanzania nje ya Nchi. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka - TDHS/MIS (2022) ambao ulikamilika na matokeo kuzinduliwa Oktoba 28, 2023, Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2024 na Utafiti wa Ajira na Mapato wa Mwaka 2023 katika Sekta Rasmi Nchini.

3.4.8 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilipanga kuendelea na ujenzi wa mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao awamu ya pili; kutoa mafunzo kwa watumishi 2,000 kutoka katika taasisi nunuzi 1,000 na wazabuni 5,000 kuhusu mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma; kufanya kaguzi ya thamani ya fedha katika taasisi nunuzi 85 na kaguzi ya ukidhi wa sheria kwa taasisi nunuzi 300; na kufanya mapitio ya nyaraka sanifu za zabuni. Aidha, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma ilipanga kutoa mafunzo kwa wajumbe, wafanyakazi wa mamlaka, wazabuni na taasisi nunuzi kuhusu utumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kusimamia rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma. Vilevile, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ulipanga kuanza ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Kigoma, na ofisi na vituo vya mafuta katika mikoa ya Njombe na Arusha pamoja na Wilaya ya Kahama, Korogwe na Masasi; kuboresha mfumo wa GIMIS ili kuwezesha matumizi ya kadi katika huduma za ununuzi wa mafuta; na kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini uwezekano na mahitaji ya kuunganisha mfumo wa GIMIS na pampu pamoja na tanki za mafuta.

63. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma - NeST awamu ya kwanza na umeanza kutumika rasmi Oktoba 2023; watumishi 12,812 kutoka taasisi 813, wazabuni 2,259 na makundi maalumu 248 wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa NeST; ukaguzi wa ukidhi wa sheria umefanyika kwa taasisi nunuzi 239, sawa na asilimia 79.7 ya lengo; na Mamlaka imefanya ukaguzi wa thamani ya fedha kwa taasisi nunuzi 89, sawa na asilimia 104.7 ya lengo. Aidha, mafunzo kuhusu utumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kushughulikia rufaa za ununuzi wa umma yametolewa kwa wajumbe na wafanyakazi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma; na jumla ya mashauri 41 yamepokelewa, kusikilizwa na kutolewa uamuzi.

64. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini umetekeleza miradi ya ujenzi katika mikoa ya Arusha (asilimia 15), Njombe (asilimia 7), Kigoma (asilimia 13) na Wilaya ya Kahama mradi upo katika hatua za awali - mobilization. Mradi wa Kigoma unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Novemba 2024, miradi ya Arusha na Njombe inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Aprili 2025 na mradi wa Korogwe upo katika hatua za ufuatiliaji wa hati ya kiwanja. Aidha, Wakala umetangaza zabuni ya uboreshaji wa mfumo wa GIMIS ili kuwezesha matumizi ya kadi katika huduma za ununuzi wa mafuta. Vilevile, katika kipindi hicho, Wakala umekamilisha andiko na hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata mshauri elekezi kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini mahitaji ya kuunganisha mfumo wa GIMIS na miundombinu ya

mafuta, yaani pampu na matenki kwa lengo la kuongeza tija na udhibiti wa huduma ya mafuta.

3.4.9 Michango ya Taasisi za Wizara katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, taasisi za Wizara ya Fedha zilitarajia kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 239.05, ikijumuisha gawio shilingi bilioni 231.20 na michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 7.85. Hadi Aprili 2024, taasisi za wizara zimechangia jumla ya shilingi bilioni 108.37, sawa na asilimia 45.33 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 100.80 zimetokana na gawio, ikiwa ni ufanisi wa asilimia 44 na michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 7.57, sawa na ufanisi wa asilimia 96.

3.4.10 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

66. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24 taasisi zilizo chini ya wizara zilitarajia kutekeleza jumla ya miradi 11 ikijumuisha ujenzi wa madarasa, maktaba, kumbi za mihadhara, migahawa, maabara za kompyuta, nyumba za watumishi na majengo ya ofisi. Hadi Aprili 2024, miradi mitatu (3) imekamilika na kuanza kutoa huduma na miradi nane (8) ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi iliyokamilika ni jengo la ofisi za makao makuu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, jijini Dodoma; na ukumbi wa mihadhara awamu ya pili na hosteli ya wanafunzi awamu ya kwanza katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Kampasi ya Dodoma na Mwanza mtawalia.

67. Mheshimiwa Spika, miradi iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni pamoja na: ujenzi wa jengo la utawala na uzio katika Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (asilimia 98); ujenzi wa jengo la utawala (asilimia 97) na utawala na taaluma (asilimia 35) katika Taasisi ya Uhasibu Tanzania Kampasi ya Mwanza na Kigoma mtawalia; ujenzi wa hosteli ya wanafunzi awamu ya tatu (asilimia 80) na hosteli ya wanafunzi awamu ya pili (asilimia 5) katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa Kampasi ya Miyuji na Mwanza mtawalia; na ujenzi wa jengo la utawala (asilimia 93) na hosteli mbili (2) za wanafunzi (asilimia 49) katika Chuo cha Uhasibu Arusha Kampasi ya Babati.

3.5 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

68. Mheshimiwa spika, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipanga kufanya ukaguzi wa rasilimali za umma kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma; kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, maalumu, kiuchunguzi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA; kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya ofisi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi mikoani.

69. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Ofisi imefanya kaguzi 1,450 ikijumuisha ukaguzi wa Serikali Kuu (537), Mamlaka za Serikali za Mitaa (625), Mashirika ya Umma (215), Ukaguzi wa Ufanisi (14), Kiufundi (10), Kiuchunguzi (7), Maalumu (12) na Mifumo ya TEHAMA (30). Aidha, Ofisi imekamilishaji kuandaa Ripoti jumuishi sita (6) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Machi 28, 2024.

3.6 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti na Mikakati ya Kukabiliana nazo

3.6.1 Changamoto

70. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2023/24, wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:
i. Huduma hafifu ya matengenezo ya mashine za EFD, kukosekana kwa mtandao na mwamko mdogo wa wananchi kudai na kutoa risiti za kielektroniki za EFD;
ii. Kuongezeka kwa mahitaji ya ziada ya rasilimali fedha kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na
iii. Baadhi ya walipakodi kuficha taarifa za miamala ya kibiashara na kuendelea kuwepo kwa biashara za magendo, hususan mipakani na mwambao wa bahari.

3.6.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto

71. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, wizara imechukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:
i. Kuhamasisha matumizi ya mfumo wa Virtual Fiscal Devices (VFD) kutoa risiti kama mbadala wa mashine za EFD;
ii. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudai na kutoa risiti za kielektroniki;
iii. Kuimarisha soko la ndani la fedha ili kuwezesha utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa kutumia vyanzo mbadala vya mapato;
iv. Kufanya mapitio ya mipango na bajeti ili kugharamia mahitaji ya ziada ya kurejesha miundombinu iliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi;
v. Kuboresha mifumo ya usimamizi wa mapato ikiwemo doria mipakani na mwambao wa bahari ili kudhibiti biashara za magendo na udanganyifu; na
vi. Kufungamanisha mifumo ya mipango na bajeti za kisekta na mifumo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**4.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25**

72. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya wizara pamoja na taasisi kwa mwaka 2023/24, sasa napenda kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/25.

73. Mheshimiwa Spika, mpango na bajeti ya wizara kwa mwaka 2024/25 umeandaliwa kwa kuzingatia sera, mikakati, sheria, mipango na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake; mikakati na makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne; Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 uliofanyiwa mapitio ya muda wa kati; na masuala mtambuka ikijumuisha jinsia, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabianchi na UKIMWI.

4.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Wizara

74. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya mafungu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:
i. Kutafuta na kukusanya mapato ya shilingi trilioni 44.19 kati ya maoteo ya shilingi trilioni 49. 35 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali;
ii. Kuimarisha na kusimamia mifumo ya mapato, matumizi na mali za Serikali ikiwemo IDRAS, TANCIS, MUSE, NeST, CBMS na GAMIS;
iii. Kuhudumia deni la Serikali kwa wakati na kuboresha kanzidata ya kutunza taarifa za deni;
iv. Kutoa elimu ya huduma za fedha kwa wananchi kwa lengo la kukuza huduma jumuishi za fedha nchini; na
v. Kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi pamoja na waratibu wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za umma.

4.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

75. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na:
i. Kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma kama yalivyoidhinishwa na Bunge mwaka 2023/24;
ii. Kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA;
iii. Kufanya kaguzi maalumu na kiuchunguzi kulingana na mahitaji;
iv. Kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga na kukarabati ofisi za mikoa; na
v. Kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi na za Kisekta ili kuzielewa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

4.3 Vipaumbele vya Taasisi za Wizara kwa Mwaka 2024/25

76. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, baadhi ya majukumu ya wizara yanatekelezwa kupitia taasisi za elimu, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi wa masuala ya fedha, kodi, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji pamoja na takwimu. Vipaumbele vya taasisi hizo kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:

4.3.1 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu

77. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/25, taasisi tano (5) za elimu zilizo chini ya wizara zinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi 86,098, ikijumuisha ngazi ya astashahada 12,450, stashahada 18,848, shahada 49,549 na uzamili 5,251. Kati ya idadi hiyo, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinatarajia kudahili wanafunzi 17,775, Taasisi ya Uhasibu Tanzania wanafunzi 30,972, Chuo cha Uhasibu Arusha wanafunzi 19,136, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini wanafunzi 16,652 na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika wanafunzi 1,563. Aidha, taasisi hizo zinatarajia kuendeleza watumishi 152 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili (26) na uzamivu (126). Vilevile, taasisi hizo zinatarajia kufanya tafiti 85 na kutoa huduma elekezi 818.

78. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka 2024/25, taasisi za elimu zinatarajia kupokea shilingi bilioni 8.94 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitano (5) inayolenga kuimarisha na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

4.3.2 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/25, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 29.42. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 28.87 ni mapato ya kodi na shilingi bilioni 541.10 ni mapato yasiyo ya kodi. Aidha, Mamlaka itaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti biashara za magendo ili kupunguza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Vilevile, Mamlaka inatarajia kupokea jumla ya shilingi bilioni 25.97 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo kuimarisha na kuboresha mifumo ya usimamizi wa mapato ya Serikali, kununua vitendea kazi na kuboresha mazingira mahali pa kazi, hususan majengo ya ofisi.

80. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/25, Bodi ya Rufani za Kodi inatarajia kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi yanayotokana na maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; kuandaa Juzuu ya Taarifa za Sheria za Kodi Tanzania; na kuhuisha Sheria ya Rufani za Kodi, Sura 408 pamoja na kanuni zake. Vilevile, Baraza la Rufani za Kodi linatarajia kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi yanayotokana na maamuzi ya Bodi ya Rufani za Kodi. Kadhalika, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi inatarajia kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya taasisi; kupokea na kutatua malalamiko ya walipakodi; kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kupokea na kuchakata malalamiko; kuratibu kutungwa kwa sheria mpya ya taasisi; na kujenga uwezo kwa watumishi katika maeneo ya uendeshaji na usuluhishi wa malalamiko.

4.3.3 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha

81. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/25, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu inatarajia kusajili wahasibu na wakaguzi wa hesabu 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kutoa mafunzo ya uandaaji na ukaguzi wa taarifa za fedha kwa wahasibu na wakaguzi 12,500; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 75; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 65 za ukaguzi; kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ngazi mbalimbali kwa awamu mbili kwa watahiniwa 14,540; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu wenye sifa za nje ya nchi wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji kwa awamu mbili kwa watahiniwa 1,451; na kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 150. Aidha, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kufanya ukaguzi wa ukidhi wa Sheria ya Bodi kwa taasisi za umma na binafsi na kuhuisha kanzidata ya wataalamu wa ununuzi na ugavi. Vilevile, Bodi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi; kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa watahiniwa 6,500; na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000.

4.3.4 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha

82. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/25, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imepanga kutoa leseni 12,456 ikijumuisha leseni mpya 1,126 na kuhuishwa leseni11,330; kufanya kaguzi 12 kwa kuzingatia vihatarishi katika michezo mbalimbali ya kubahatisha; kutekeleza operesheni nne (4) za kutokomeza michezo haramu ya kubahatisha; kukusanya mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha ya jumla ya shilingi bilioni 24.89; kuendelea kuelimisha jamii juu ya athari hasi za michezo ya kubahatisha; na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

4.3.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

83. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mitaji ubia (venture capital); kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida za masoko ya mitaji; kuidhinisha bidhaa mpya mbili (2) kuwezesha taasisi na kampuni katika sekta ya umma na binafsi kupata fedha za kugharamia biashara na miradi ya maendeleo; na kuboresha mifumo ya usimamizi wa shughuli za masoko ya mitaji. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania linatarajia kuanza ujenzi wa jengo la ofisi makao makuu Dar es Salaam lenye thamani ya shilingi bilioni 8.35 ikiwa ni ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

4.3.6 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

84. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo mpya unaotumia riba ya benki kuu. Kulingana na mwenendo wa uchumi wa dunia, utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25 unatarajiwa kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kuwa ndani ya lengo la asilimia 5; kudhibiti kiwango cha riba za mikopo ya siku saba (7) baina ya benki; kudhibiti mwenendo wa sera ya fedha ili kunaendana na malengo ya utekelezaji wa programu ya Extended Credit Facility (ECF); kufuatilia taasisi za fedha kupanga riba na viwango vya kubadilisha fedha kwa kuzingatia nguvu ya soko; na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya benki ili kudhibiti akiba ya fedha za kigeni.

85. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 56.54; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 20.83 kutoka shilingi bilioni 18.79 ya mwaka 2023; kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 197 ikilinganishwa na shilingi bilioni 161.6 zilizotolewa mwaka 2023; kuongeza thamani ya mali za Benki kufikia shilingi bilioni 866.23 kutoka shilingi bilioni 606.94 mwaka 2023; na kufuatilia marejesho ya mikopo shilingi bilioni 70 kutoka kwa wateja.

86. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024, Benki ya Maendeleo TIB imepanga kuongeza mtaji wa benki hadi shilingi bilioni 204.61 kutoka shilingi bilioni 86.61 mwaka 2023; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 89.02 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.74 mwaka 2023; kuongeza mali za benki hadi shilingi bilioni 545.48 kutoka shilingi bilioni 425.15 mwaka 2023; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya benki shilingi bilioni 17.44 na mkopo iliyoko katika mizania ya benki shilingi bilioni 30.38; na kusimika mifumo mitatu (3) ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

87. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024, Benki ya Biashara Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 225; kukuza faida ya benki kabla ya kodi shilingi bilioni 37.3; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 1,173; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,340; kukuza mali za benki hadi shilingi bilioni 1,701 kutoka shilingi bilioni 1,389.3 mwaka 2023; kukuza mtaji wa benki hadi shilingi bilioni 147 kutoka shilingi bilioni 118.9 mwaka 2023; kuongeza idadi ya wateja hadi 881,122 kutoka wateja 831,122 mwaka 2023; na kukamilisha uundaji na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo.

88. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF unatarajia kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi bilioni 48 kwa wajasiriamali 48,000; kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 3.28 kutoka shilingi bilioni 1.89 mwaka 2023; kukuza mtaji hadi shilingi bilioni 65.48 kutoka shilingi bilioni 61.14 mwaka 2023; kuongeza idadi ya wateja hadi 48,000 kutoka wateja 37,024 mwaka 2023; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya mfuko shilingi bilioni 2 na mikopo iliyo katika mizania shilingi bilioni 48.53; na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 11.03.

89. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS inatarajia kuongeza rasilimali za mifuko hadi shilingi bilioni 2,642.7 kutoka shilingi bilioni 2,012.8 mwaka 2023/24; kuongeza idadi ya wawekezaji hadi 367,500 kutoka 310,806 mwaka 2023/24; na kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 28.03 kutoka shilingi bilioni 18.82 mwaka 2023/24.

90. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inatarajia kujenga mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya tozo za ada ya bima; kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi jijini Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 3.80; kufanya ukaguzi kwa wadau wa bima 259 (kampuni 25 na matawi 30, madalali 66, mawakala 150, benkiwakala10 na matawi 20 na wauza bima kidijiti nane (8)); kuchambua mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 36; kutoa elimu ya bima kwa umma; kuidhinisha bidhaa mpya tano (5) zinazokidhi mahitaji ya watu wenye kipato cha chini; na kuongeza wasajili wapya wa bima 105.

91. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Shirika la Bima la Taifa linatarajia kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu bidhaa na huduma za shirika; kuboresha utoaji huduma kwa wateja kupitia uandikishaji wa Cheti cha Ubora (ISO 9001:2015) katika ofisi 11 za kanda; kupunguza muda wa malipo ya madai kutoka siku 16 hadi saba (7); kuongeza wateja wapya 324 wa bidhaa za taasisi kutoka wateja 222 mwaka 2023/24; kubuni bidhaa mpya mbili (2) na kuboresha bidhaa tatu (3) kuendana na mahitaji ya soko; kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 85.57 kutoka shilingi bilioni 51.42; na kuongeza mapato ya taasisi kutoka shilingi bilioni 244.34 hadi shilingi bilioni 314.78.

4.3.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

92. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatarajia kuendelea na jukumu lake la msingi la kutoa takwimu rasmi za kijamii, kiuchumi na mazingira kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Takwimu, SURA 351. Aidha, shabaha nyingine ni kuchambua, kusambaza na kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika ngazi ya halmashauri, majimbo, kata, shehia, mtaa, kijiji hadi kitongoji; kuendelea na Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2024; Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na Ufuatiliaji wa Kaya wa Mwaka 2024/25; Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2023/24; na kufanya Sensa ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar inatarajia kujenga majengo ya ofisi katika mikoa ya Pemba, Lindi na Simiyu kwa gharama ya shilingi bilioni 3.4 kila moja kwa ajili ya kuhudumia mkoa wa Pemba, Kanda ya Kusini na Kanda ya Ziwa. Kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatarajia kujenga kituo cha kisasa cha kuchakata takwimu Jijini Dodoma.

4.3.8 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

93. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma inatarajia kukamilisha ujenzi wa moduli tatu (3) za mfumo wa NeST; kufanya tafiti tatu (3) kuhusu matumizi ya fomula ya mabadiliko ya bei katika miradi ya ujenzi, ununuzi endelevu na matumizi ya force account, na ununuzi kwa njia ya mzabuni mmoja ikilinganishwa na ushindani; kuandaa na kupitia nyaraka sanifu 42 na miongozo tisa (9) ya ununuzi wa umma kwa matumizi ya taasisi nunuzi; kutoa elimu kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa watumishi 8,160 kutoka katika wizara, taasisi za serikali, sekretarieti za mikoa na halmashauri, wazabuni 4,000, asasi za kiraia 100, makundi maalumu 110 na wanafunzi 4,000 wa vyuo vikuu; na kufanya ukaguzi wa ununuzi kwa taasisi nunuzi 500.

94. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma imepanga kusajili na kusikiliza rufaa 55; kutoa mafunzo kwa wazabuni 800 kuhusu moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa; na kutoa mafunzo kwa wakuu wa idara/vitengo 300 vya ununuzi na sheria kuhusu usimamizi wa malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki. Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini unatarajia kununua magari manne (4) ya kusafirishia mafuta; kuunganisha mfumo wa GIMIS na pampu na matenki ya mafuta; na kuanzisha utoaji wa huduma za mafuta kwa kutumia kadi kupitia mfumo wa GIMIS. Aidha, Wakala unatarajia kujenga ofisi, ghala na kituo cha mafuta katika Wilaya ya Mbarali (Mbeya), Masasi (Mtwara), Korogwe (Tanga) na Jiji la Arusha; na ujenzi wa ofisi ya Mkoa Dar es Salaam.

4.3.9 Michango ya Taasisi za Wizara katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

95. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, taasisi za Wizara ya Fedha zinatarajia kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 233.99. Kati ya kiasi hicho, gawio ni shilingi bilioni 224.15 na mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 9.84.

4.4 Mapendekezo ya Bajeti ya Mafungu ya Wizara na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2024/25

4.4.1 Mapato

96. Mheshimiwa Spika, kati ya shilingi trilioni 49.35 zinazokadiriwa kukusanywa na Serikali kwa mwaka 2024/25, Wizara ya Fedha imekadiriwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 44.19. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 29.42, misaada na mikopo nafuu shilingi trilioni 5.13, mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje shilingi trilioni 9.60 na maduhuli shilingi bilioni 45.01. Aidha, Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inakadiria kukusanya shilingi milioni 850 ikiwa ni mapato ya kodi ya pango kutokana na upangishaji wa majengo ya Ofisi yaliyopo katika mikoa mbalimbali nchini.

4.4.2 Matumizi

97. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/25, Wizara ya Fedha inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi trilioni 18.17 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu nane (8) ya kibajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 17.63 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha huduma ya deni la Serikali shilingi trilioni 13.13, mishahara shilingi bilioni 946.45, matumizi mengineyo shilingi bilioni 937.30 kwa mafungu ya wizara na taasisi zake, Huduma za Mfuko Mkuu shilingi trilioni 2.61 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 544.05. Aidha, ninaomba Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iidhinishiwe jumla ya shilingi bilioni 112.73 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 101.26 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11.47 matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi kwa mafungu nane (8) ya kibajeti ya Wizara ya Fedha na Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi umeoneshwa katika Jedwali Na.1 na mchanganuo wa kina katika Kiambatisho Na.4

**5.0 HITIMISHO**

98. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb,), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha, nawashukuru watendaji wakuu wa wizara na taasisi zake wakiongozwa na Dkt. Natu E. Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bi. Jenifa C. Omolo na Bw. Elijah G. Mwandumbya kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya wizara na taasisi. Vilevile, nawashukuru wakuu wa idara, vitengo na wafanyakazi wote wa wizara na taasisi zake, kwa ushirikiano na utekelezaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku. Asanteni sana na Kazi Iendelee.

99. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu pamoja na waheshimiwa wabunge na umma wa watanzania kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya wizara ambayo ni www.mof.go.tz.

100. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

## Rasmi ANC yaanza mazungumzo kuunda muungano

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MAZUNGUMZO ya faragha kati ya Chama cha 'African National Congress' (ANC) pamoja na vyama vingine vidogo vya upinzani yameanza nchini Afrika Kusini kwa lengo la kuunda muungano, huku bunge likitarajia wiki mbili mbele kumteua mkuu wa nchi ajae.

Wakati huo huo, viongozi wakuu wa ANC wanatarajiwa kukutana wiki hii katika makao makuu ya chama hicho jijini Johannesburg. Miongoni mwao, wakiwa ni Rais Cyril Ramaphosa, kiongozi wa chama, pamoja na naibu wake.

Ilielezwa kuwa kutokana na kupotea kwa wingi kamili wa viti katika bunge la taifa wakati wa uchaguzi mkuu, majadiliano yanapaswa yazingatie uwezekano wa muungano na upinzani.

Licha ya hasara kubwa ya wapigakura, ANC kinasalia kuwa chama kikuu cha siasa nchini Afrika Kusini, chenye viti vingi zaidi bungeni, huku uchaguzi wa rais ukibakia kwa kiasi kikubwa ndani ya uwezo wake, wakati kiongozi wa taifa hilo Ramaphosa akiwania muhula wa pili.

Baada ya kutangaza matokeo rasmi juzi na kutoa hotuba ya maelewano, iliyothaminiwa sana na wananchi wa taifa hilo, Rais Ramaphosa atavaa vazi la kiongozi wa chama chake. Na kwamba anapaswa kuzungumza mwishoni mwa mazungumzo ya kuwashukuru wapigakura milioni sita wa ANC.

Watafiti walieleza kuwa endapo ANC itaelewana na Chama cha Democratic Alliance (DA), kungekuwa na uhakika wa utulivu wa nchi, hasa kwenye mtazamo wa kiuchumi. Licha ya kudaiwa kuwa suluhisho bado haliwezekani, huku wengine wakieleza kuwa hiyo inaweza kutoa hoja kwa wale wanaoshutumu ANC kuwa inapendelea ulimwengu wa biashara ambao wengi wao ni wazungu.

Katika mchakato wa muungano chama cha mrengo wa kushoto cha Julius Malema, kilichoshika nafasi ya nne, kimeonyesha kuwa kiko tayari kufanya kazi na ANC, pamoja na MK chama kipya cha Jacob Zuma, ambacho kilishika nafasi ya tatu, kinachomtaka Rais Ramaphosa ajiuzulu kabla ya majadiliano yoyote.

Katibu Mkuu wa Chama cha ANC, Fikile Mbalula, alisema wana mashaka na kuhusu pendekezo la MK lakini wanaendelea kuzungumza na kila mtu, na kwamba uamuzi wa viongozi wakuu wa ANC utaidhinishwa na kamati kuu ya utendaji.

Kamati iliyokusanyika tayari imedokeza kuwa haina nia ya kujitenga na kiongozi wake, Rais Ramaphosa, mgombea kwa muhula wa pili. **RFI**

# Benki Uingereza yashutumiwa kufadhili makundi ya ugaidi

**LONDON,** Uingereza

MAHAKAMA ya Marekani imedai kwamba Benki ya Uingereza iliyokwepa kushtakiwa kwa utakatishaji fedha ilifanya miamala ya mabilioni ya dola kwa wafadhili wa makundi ya kigaidi.

Ilielezwa jana kwamba Standard Chartered, mojawapo ya benki kubwa zaidi za Uingereza, iliepuka kufunguliwa mashtaka na Idara ya Sheria ya Marekani baada ya serikali ya David Cameron kuingilia kati kwa niaba yake mwaka 2012.

Nyaraka mpya zilizowasilishwa kwenye mahakama ya New York zinadai maelfu ya miamala yenye thamani ya zaidi ya dola bilioni 100 (Sh. Trilioni 259.1) ilifanywa na benki hiyo kutoka 2008 hadi 2013 kwa kukiuka vikwazo dhidi ya Iran.

Mtaalamu huru alibainisha kwamba dola bilioni 9.6 (Sh. Trilioni 25) ya miamala ya fedha za kigeni za watu binafsi na makampuni yalibainika na serikali ya Marekani kama yanafadhili makundi ya kigaidi, ikiwa ni pamoja na Hezbollah, Hamas, al-Qaeda na Taliban.

Katika taarifa ya benki hiyo ilisema inapinga madai ya watoa taarifa, ikisema madai yao ya awali yalipuuzwa kabisa na mamlaka ya Marekani.

**YALIYOKIUKWA**

Ilielezwa kuwa Standard Chartered ilishutumiwa hadharani kwa kughushi data ya muamala kwenye mfumo wa malipo wa kimataifa unaotumiwa na maelfu ya mashirika ya kifedha kuhamisha mabilioni ya dola kupitia tawi lake la New York kwa niaba ya mashirika yaliyoidhinishwa kama vile Benki Kuu ya Iran.

Lakini Septemba 2012, George Osborne, aliyekuwa kansela katika serikali ya David Cameron, aliingilia kati kwa siri kwa niaba ya benki hiyo, na kwamba miezi mitatu baadae, Idara ya Haki ya Marekani iliamua kutoishtaki benki hiyo.

Shughuli za ubadilishanaji fedha za kigeni zilizoainishwa katika faili za mahakama zilikuwa bado hazijajulikana na haikuchukuliwa kuwa Osborne au Cameron walikuwa na ujuzi wowote wa shughuli hizi wakati huo.

Benki hiyo ilikiri mara mbili kukiuka vikwazo dhidi ya Iran na nchi nyingine mwaka 2012 na 2019 na kulipa faini ya jumla ya zaidi ya dola bilioni 1.7 (Sh. Trilioni 4.4) lakini haijakubali kufanya shughuli za miamala kwa mashirika ya kigaidi. **BBC**



Baadhi ya wakazi katika Ukanda wa Gaza wakitazama makazi yao yaliyoharibiwa vibaya na mashambulizi ya Israel. **PICHA: MTANDAO**

# Mfanyakazi wa hospitali ya rufani adaiwa kuuawa na askari wa JKU

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MFANYAKAZI wa Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja, Said Ali Shineni (45) anadaiwa kuuawa kwa kushambuliwa na askari wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Zanzibar waliokuwa katika lindo hospitalini huko.

Tukio hilo ambalo limezua mjadala visiwani huku familia ya marehemu ikigoma kuzika mwili wa mpendwa wao, ilidaiwa kutokea juzi saa tatu usiku katika hospitali hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Muhiddin Abdi Mahmoud, alisema uongozi umepokea taarifa kwamba mtumishi wao huo aliuawa akiwa katika mikono mwa askari usiku wa kuamkia jana.

Alisema kuwa askari hao walimshikilia kwa lengo la kumkabidhi kwa Jeshi la Polisi ili kuchukuliwa hatua za kijinai kufuatia tuhuma za kutenda kosa la wizi.

Mkurugenzi huyo alisema mwili wa marehemu umo katika chumba cha kuhifadhia maiti hospitalini huko kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi ili kubaini kifo chake kinatokana na shambulio au la.

"Taarifa kamili juu ya kifo chake itatolewa baada tu ya kupatikana ripoti kamili ya chama hicho kupitia mamlaka husika," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema hakuna taarifa za awali kwamba marehemu wakati wa uhai wake alikuwa na matukio ya wizi na hawakuwa na taarifa kwamba mtumishi wao huyo alikuwa mraibu wa dawa za kulevya kama inavyodaiwa mtaani.

Alisema uongozi wa hospitali hiyo unatoa pole kwa ndugu na jamaa wa wafanyakazi wote wa hospitali hiyo, akiwataka kuwa na subra katika kipindi hiki.

Familia yake imesema imepokea kwa masikitiko kifo cha ndugu yao huyo na haiko tayari kupokea mwili wa marehemu kwa ajili ya mazishi hadi pale uchunguzi utakapokamilika.

Adil Suleiman Sheha, mmoja wa wanafamilia, alisema alipata taarifa ya kifo hicho jana saa mbili asubuhi, kukiwa na madai kwamba ndugu yao huyo amepigwa na askari waliokuwa wanalinda hospitali hiyo.

"Tumesema hatuwezi kuchukua mwili wa marehemu mpaka tupate ripoti kamili ya daktari kuwa kifo chake kimesababishwa na nini," alisema Sheha ambaye ni mjomba wa marehemu.

Aliomba serikali kama uchunguzi utabainika kuwa kifo cha ndugu yao kinatokana na tuhuma zilizopo za kupigwa, ichukue hatua stahiki kwa waliotenda kosa hilo.

Alisema kitendo cha wizi hakihusiani na kukatishwa uhai wa ndugu yao. Kama alikuwa anakabiliwa na tuhuma hizo, alipaswa kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zinazostahiki.

Marehemu Shineni alikuwa mkaazi wa Tomondo, Wilaya ya Magharib B Unguja na mtumishi wa serikali katika Wizara ya Afya, Idara ya Uhudumu Hospitali ya Mnazi Mmoja.

# BOSI WA WAAMUZI AFUNGUKA ARAJIGA KUPATA MECHI KUBWA

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Waamuzi wa Soka Tanzania imesema mwamuzi, Ahmed Arajiga, amekuwa na kiwango bora zaidi msimu huu, ndiyo maana amekuwa akipewa mechi zenye mvuto kwa mashabiki na zinazotazamwa na idadi kubwa ya wadau wa ndani na nje ya nchi.

Arajiga amechezesha mechi zote mbili za watani wa jadi msimu uliomalizika, akisimama kati pia katika Fainali ya Kombe la Muungano na Jumapili iliyomalizika alisimamia fainali ya FA iliyowakutanisha Yanga na Azam FC. Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Nassor Hamduni, alisema ubora wa mwamuzi huyo kutoka Manyara ndio siri kubwa ya kuteuliwa katika kuchezesha mechi nyingi msimu huu.

Hamduni alisema wamekuwa na waamuzi wengi wazuri, lakini kwa msimu huu, Arajiga ameonyesha kiwango bora, ukichanganya na uzoefu aliokuwa nao wamekuwa wakilazimika kumpanga na hajawaangusha.

"Ni kweli Arajiga amekuwa na msimu bora kabisa, pamoja na kina, Frank Komba, Mohamed Mkono, Kassim Mpanga, Janeth Balama, Amina Kyando, Tatu Malogo, tunao wengi tu wazuri, ila yeye ndiyo mfano wa waamuzi nchini.

Katika mechi zinazotazamwa na watu wengi ndani na nje ya nchi, lazima tupange waamuzi wazuri, wenye uwezo wa ujasiri wa kusimamia mchezo na siyo hatuna waamuzi wengine, lengo ya TFF na Kamati ya Waamuzi ni kuhakikisha michezo hiyo inaisha bila matatizo ya hapa na pale.

Hivyo huwezi kuwapa vijana kwa sababu yakitokea matatizo kidogo, yanaweza kuwatoa kwenye njia yao ya kwenda katika mafanikio, kuliko wale ambao ni wazoefu," alisema Hamduni.

Alitoa mfano Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) na lile la Dunia (FIFA), pia kuna waamuzi ambao wanajirudia, na mara nyingi ni wale wazoefu.

Hata hivyo aliongeza kwa muda wa miaka miwili wametengeneza waamuzi wengi, ambao wataanza kuonekana msimu ujao, huku waamuzi waliozoeleka wakionekana mara chache.

"Naamini msimu unaokuja mtashuhudia waamuzi wengi wapya, na mtaona mapumziko ya hawa wakubwa katika mechi kubwa, ila si kama Arajiga, hawatachezesha kabisa mechi mnazoziita kubwa, lakini zitapungua.

Niwaambie tu sisi kwetu hatuna mechi kubwa na wala hatuziiti hivyo, kwa sababu sheria ni hizo hizo, ila tunafanya hivyo kwa sababu zinatazamwa na kufuatiliwa na mashabiki wengi," alisema bosi huyo wa waamuzi.



Wachezaji wa Bunda Queens wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Yanga Princess kutoka Dar es Salaam itakayochezwa keshokutwa Mjini Musoma mkoani Mara. **PICHA: MTANDAO**

# Mtanzania aula netiboli Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa timu ya taifa ya vijana ya netiboli, Macklina Mwita, amepata fursa ya kwenda Afrika Kusini kushiriki mafunzo mbalimbali pamoja na masomo chini ya usimamizi wa shirikisho la mchezo huo Afrika (IFNA), imeelezwa.

Macklina amepata nafasi hiyo baada ya kuonyesha kiwango kizuri katika mashindano ya vijana ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia yaliyofanyika Machi, mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Devotha Marwa, alisema hiyo ni habari njema kwa nchi na itafungua milango kwa wachezaji wengine kupata nafasi ya kwenda kujiendeleza.

"Mchezaji wetu (Macklina), alionyesha uwezo mkubwa katika mashindano hayo ambayo yalikuwa na upinzani, hatimaye amepata bahati kubwa kama hiyo," alisema Devotha.

Aliongeza anawaomba wazazi na walezi kuwaruhusu watoto wao kushiriki katika mashindano mbalimbali ya taifa ili wapate kujulikana kirahisi.

"Ninaomba wazazi wawaruhusu watoto wao kunapotokea fursa kama hizi, michezo ni ajira vilevile hujenga afya," alisema mwenyekiti huyo.

Aliongeza huu ni wakati kwa wachezaji wengine kuongeza bidii katika timu zao ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kupata ufadhili wa masomo na michezo.

## KMKM SC yakubali 'kuutema' ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KMKM SC imesema haina matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kupoteza mechi dhidi ya Mafunzo na kuwaacha wapinzani wao JKU wakijiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

KMKM iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 55, kila timu imebakisha michezo mitatu ili kukamilisha msimu wa 2023/24.

Kocha Mkuu wa KMKM SC, Ame Msimu, aliliambia gazeti hili anasikitika kuona wameshindwa kufikia malengo ya kutetea taji walilokuwa wanalishikilia.

"Kutokana na msimamo wa ligi ulivyo, ili sisi kutwaa ubingwa ni mpaka mpinzani (JKU), wetu afungwe michezo yote mitatu iliyobakia na sisi tushinde michezo hiyo ya mwisho, ni jambo ambalo haliwezekani ingawa katika soka lolote linaweza kutokea," alisema Msimu.

Aliongeza ligi ya msimu huu imekuwa na ushindani zaidi na kupelekea kikosi chake kushindwa kutetea taji na kutinga fainali ya Kombe la FA, lakini wataendelea kuhamasisha wachezaji na mashabiki ili kupata matokeo chanya na kumaliza msimu salama.

## Wanawake Mwanza kuchaguana J'mosi

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

CHAMA cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Mwanza kinatarajia kufanya uchaguzi wa viongozi Jumamosi, imeelezwa.

Taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Chama cha Soka Mwanza (MZFA), Mussa Nyamwelo, imewataja wanaogombea nafasi ya Mwenyekiti ni Sophia Makilagi na Sophia Tigalyoma.

Nyamwelo aliwataka wagombea watakaochuana katika nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa (TWFA), ni Johari Ngassa na Revina Muzawena.

Alisema pia wagombea wanne wamejitokeza kuwania nafasi mbili za Ujumbe wa Kamati ya Utendaji ambao ni pamoja na Elizabeth Nyingi, Glory Mbise, Flora Gaguti na Hawa Bajanguo.

"Taratibu zote zimefuata kuelekea uchaguzi huu, tunawakumbusha wagombea na wadau wote kuhakikisha wanafanya kampeni kistaarabu, tunaamini tutamaliza mchakato huu kama ilivyotarajiwa," alisema Katibu Mkuu wa MZFA, Leonard Malongo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALISON ATAJWA SAUDIA

KIPA wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Brazil, Alisson, mwenye umri wa miaka 31, ametambuliwa na Saudi Pro League kama mmoja wa walengwa wao wakuu msimu huu wa joto. (***Teamtalk***)

### VILLA YAMTAKA BARKLEY

KLABU ya Aston Villa inatazamia kukamilisha dili la pauni milioni tano ili kumsajili kiungo wa kati wa Uingereza, Ross Barkley, mwenye miska 30, kutoka Luton Town. ***(talkSPORT)***

### NKETIAH NJIA MOJA

ARSENAL itamruhusu mchezaji wa kimataifa wa England, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 25, kuondoka katika klabu hiyo kwa ‚shingo upande' huku Fulham wakiwa tayari kutoa karibu pauni milioni 30 kwa ajili ya fowadi huyo, ambaye anazivutia Crystal Palace, Wolves na Everton. (***Sun***)

### ARSENAL, BAYERN VITANI

ARSENAL iko tayari kutoa ofa kwa beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Ukraine, Oleksandr Zinchenko, mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akihusishwa na Bayern Munich. (***Football Insider***)

### SUMMERVILLE SOKONI EPL

WINGA wa Leeds United ambaye ni raia wa Uholanzi, Crysencio Summerville, ameonekana kuwa katika rada za Liverpool ambaye thamani yake ni pauni milioni 30.(***Mirror)***

### BELLINGHAM HAUZWI NG'O

KLABU ya Sunderland imedhamiria kutomuuza mchezaji wa kimataifa wa England, Jobe Bellingham mwenye miaka 18, huku Tottenham, Brentford na Crystal Palace zikimhitaji kiungo huyo. (***Guardian***)

### INACIO AGOMBEWA ENGLAND

KLABU za Manchester United na Liverpool zinamfuatilia beki wa kati wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Goncalo Inacio, mwenye umri wa miaka 22. (***Fabrizio Romano***)

### SANCHO KUREJEA DORTMUND

WINGA wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24, atashinikiza kurejea Dortmund kwa mkataba wa kudumu kutoka Manchester United msimu huu. (***Star***)

### MADRID YAMNASA JOSELU

REAL Madrid wameamua kutumia chaguo lao kumsajili fowadi wa Hispania, Joselu, mwenye miaka 34, kwa mkataba wa kudumu kutoka Espanyol . (***The Athletic***)

### ENDO ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanapanga kumsajili kiungo mpya, huku mchezaji wa kimataifa wa Japan, Wataru Endo, mwenye umri wa miaka 31, akitazamwa kama mchezaji wa kushikilia nafasi hiyo kwa muda tu. (***Football Insider***)

### CHELSEA YAMBANA MAATSEN

KLABU ya Borussia Dortmund haina chaguo la kwanza la kumnunua kwa mkopo mlinzi wa Uholanzi, Ian Maatsen, mwenye umri wa miaka 22, huku kipengele cha Chelsea cha pauni milioni 35 kikiwa kimefunguliwa kwa timu yoyote inavyomtaka beki huyo wa kushoto.(***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RASMI MBAPPÉ MALI YA MADRID

**MADRID,** Hispania

### Mshambuliaji huyo amepewa mkataba wa miaka mitano wenye...

REAL Madrid imetangaza rasmi kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappé, kwa uhamisho wa bila malipo, hivyo basi kuhitimisha kusubiri kwa miaka mingi kumtaka ajiunge na klabu hiyo.

„Real Madrid C. F. na Kylian Mbappe wamefikia makubaliano ambapo atakuwa mchezaji wa Real Madrid kwa misimu mitano ijayo," mabingwa hao wa Hispania walisema katika taarifa yao.

Mbappé alitangaza mwezi uliopita ataondoka Paris Saint-Germain mwishoni mwa msimu mkataba wake utakapomalizika.

„Ndoto imetimia, nina furaha sana na ninajivunia kujiunga na klabu ya ndoto yangu," alisema Mbappé kupitia chapisho lake ukurasa wa X.

„Hakuna mtu anayeweza kuelewa jinsi nilivyofurahi kwa sasa. Siwezi kusubiri kukuona wana Madridista. Hala Madrid!"

Vyanzo vimeiambia ESPN Mbappé ametia saini mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya Euro milioni 15 kwa mwaka baada ya kodi, amekuwa katika mazungumzo na Madrid tangu Februari, mwaka huu.

Madrid ndio mabingwa watetezi wa LaLiga na walinyanyua Kombe lao la 15 la Ulaya Jumamosi iliyopita walipoilaza Borussia Dortmund mabao 2-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Wembley.

Mnamo mwaka, 2017 baada ya kutoka Monaco, Mbappé alikaribia kujiunga na wababe hao wa Hispania, lakini akachagua kujiunga na PSG badala yake baada ya klabu hiyo kukubaliana na dili la rekodi lenye thamani ya Euro milioni 180.

Mbappé aliendelea kuwa nahodha wa PSG na mfungaji bora wa muda wote akiwa na mabao 255, akishinda mataji sita ya Ligue 1 katika misimu saba.

Alishinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018 na alifunga hat trick katika fainali yao ya Kombe la Dunia dhidi ya Argentina ya Lionel Messi nchini Qatar miaka minne baadaye.

Mbappé hakuiongoza PSG kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kupoteza fainali pekee aliyocheza mwaka wa 2020. Pia alishindwa kufunga katika mechi zote mbili za nusu fainali dhidi ya Dortmund msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye tayari ni mfungaji bora wa tatu katika historia ya Ufaransa, pia alikaribia kujiunga na Madrid miaka miwili iliyopita.

Fowadi huyo anajiunga na Madrid ambayo tayari inajivunia nyota kama Vinícius Júnior, Jude Bellingham na Rodrygo katika safu ya ushambuliaji.

Mbappé ataiongoza Ufaransa kutwaa ubingwa wa tatu wa Ulaya katika michuano ya majira ya joto itakayofanyika Ujerumani, lakini aliachwa kwenye kikosi cha awali kilichoitwa kuwakilisha Les Bleus kwenye Michezo ya Olimpiki itakayochezwa Paris hivi karibuni.

# UNITED YASHIKILIA HATIMA YA SANCHO




**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inajiandaa kufanya mazungumzo na Jadon Sancho kabla ya kuamua juu ya mustakabali wa nyota huyo, chanzo kiliiambia ESPN.

Sancho hajaichezea United tangu Agosti, mwaka huu kufuatia mzozo wa hadharani na Kocha Erik ten Hag.

Alitolewa kwa mkopo kwa klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund mnamo Januari na kuisaidia timu hiyo ya Bundesliga kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo wikendi iliyopita walifungwa mabao 2-0 na Real Madrid.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN United wanataka kuzungumza na Sancho kabla ya kuamua ni hatua gani wachukue msimu huu wa joto.

Mkurugenzi wa Ufundi, Jason Wilcox, na Mkurugenzi wa Mazungumzo ya Soka, Matt Hargreaves, wanatazamiwa kujadili hali hiyo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 na wawakilishi wake kabla ya kuanza kwa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya.

Wachezaji wa United ambao hawajashiriki katika michuano ya kimataifa msimu huu wa joto wanatarajiwa kurejea katika klabu hiyo Julai kabla ya mechi yao ya kwanza ya kirafiki dhidi ya Rosenborg itakayochezwa Julai 15, mwaka huu huko Norway.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN hoja inasalia matokeo yanayowezekana zaidi, ingawa thamani kubwa ya soko ya Sancho na mshahara mkubwa kufanya uhamisho wake wa kudumu kuwa mgumu.

Dortmund wana nia ya kumsajili tena mshambuliaji huyo raia wa England, lakini wanataka kufanya mazungumzo ya mkataba mwingine wa mkopo na Sancho, ambaye yuko chini ya mkataba United hadi mwaka 2026, yuko tayari kujiunga tena na timu hiyo ya Ujerumani.

Wilcox na Hargreaves wanaongoza dirisha la majira ya kiangazi la United huku klabu ikisubiri kumteua rasmi, Dan Ashworth, kama mkurugenzi wao mpya wa michezo.

Juhudi za kumleta Ashworth zimekwamа kwa sababu ya madai ya Newcastle United ya kulipwa fidia ya zaidi ya pauni milioni 20.

Kikosi cha kusajili cha United kimeandaa orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kuimarisha maeneo yote ya kikosi huku beki wa kati, kiungo wa kati na mshambuliaji wakipewa nafasi za kipaumbele.

## Nitalipaisha soka la Uturuki - Mourinho

**ANKARA,** Uturuki

JOSE Mourinho alisema katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari wa Fenerbahce usajili wake na heshima kutaleta umakini zaidi katika Ligi ya Uturuki, na kuongeza lengo lake ni kushinda Super Ligi na kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

„Mojawapo ya mambo, nitaleta umakini. Watu wengi zaidi barani Ulaya watafuatilia Ligi ya Uturuki,“ alisema Mourinho.

„Ninakuja kufanya kazi kwa soka la Uturuki, kwa Ligi ya Uturuki ‚Super Lig‘. Lakini kimsingi nakuja Fenerbahce.

„Matamanio yangu ni soka la Uturuki liimarishwe katika kila ngazi. Lakini kama itabidi nipaze sauti yangu kuitetea Fenerbahce sitafikiria mara mbili,“ aliongeza, akimaanisha malalamiko ya klabu hiyo juu ya kile inachokiita ukosefu wa haki.

Super Lig ilikumbwa na utata msimu uliopita, huku kukiwa na vurugu na mizozo iliyofunika pambano la kuwania taji kati ya Fenerbahce na wapinzani wao Galatasaray.

Mourinho, ambaye ametia saini mkataba wa miaka miwili na Fenerbahce, ikiwa imepita miezi sita baada ya kutimuliwa na Roma, hakutoa ahadi kwa mashabiki wa Fenerbahce kuhusu mataji lakini ameahidi kuvaa jezi hiyo kama ni „ngozi yangu.“

Fenerbahce hawajashinda taji hilo tangu msimu wa 2013-14, na taji lao la mwisho lilikuwa Kombe la Super Cup la Uturuki mnamo mwaka 2014.




# Ronaldo afurahia msimu bora Saudia

**LISBON,** Ureno

CRISTIANO aliutaja msimu wake wa kwanza kamili kwenye Ligi ya Saudia ni „moja ya bora“ katika maisha yake baada ya kupokea tuzo kwa kufunga mabao mengi zaidi kwenye ligi hiyo, iliyovunja rekodi ya magoli 35.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alisajiliwa na Al Nassr Desemba 30, 2022, na alicheza nusu ya pili ya msimu wa SPL mnamo 2023.

Katika msimu wake wa kwanza kamili huko Saudi Arabia mnamo 2023-24, Ronaldo alivunja rekodi ya ligi ya mabao 34 iliyowekwa na Abderrazak Hamdallah, msimu wa mwaka 2018-19.

„Kusema ukweli ina maana kubwa kwa sababu ni kazi yangu,“ alisema Ronaldo.

„Lazima niwe mkweli na kusema sio kitu ambacho nilikuwa nikitafuta mwanzoni mwa msimu lakini baada ya muda nilianza kuona inawezekana, nina nafasi ya kusema asante kwa wachezaji wenzangu kwa sababu bila timu hakuna kitu ambacho kingewezekana.

Ninajisikia fahari sana kushinda rekodi ya Ligi ya Saudia. Ni jambo zuri kwangu, najisikia furaha na hii ndiyo motisha yangu ya kucheza soka, kufanya mazoezi kila wakati na kuendelea hivyo.“

Licha ya sifa hizo za kibinafsi, ulikuwa msimu usio na taji kwa Ronaldo na Al Nassr, ambao walishika nafasi ya pili kwenye Ligi ya SPL nyuma ya Al Hilal, na kushindwa kushinda kombe lolote la Ligi ya Mabingwa Asia, Saudi Super Cup na Saudi King's Cup.

Ilikuwa ni matokeo duni kwa mshindi mara tano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Ronaldo baada ya kuhamia kwake SPL akitoka Manchester United, Real Madrid na Juventus.

Ronaldo sasa ataungana na wachezaji wenzake wa Ureno kabla ya michuano ya Euro msimu huu wa kiangazi, huku mabingwa hao wa 2016 wakipangwa dhidi moja na Jamhuri ya Czech, Uturuki na Georgia.

„Nadhani malengo ya kila msimu ni ya aina moja, ni kufanya uwezavyo na kushinda mataji. Ikiwezekana, kukusanya makombe binafsi pia lakini lengo langu ni kuwa sawa, kuwa Cristiano yule yule.

## Straika wa Uganda kutua Msimbazi

INATOKA UK. 24

chetu.

Straika huyo alichukua tuzo ya mchezaji bora wa mashabiki wa Uganda, anatajwa ni mmoja wa mastraika ambaye huenda akawa mbadala wa Freddy Michael au Pa Omari Jobe, ambao hatima yao ndani ya kikosi cha Wekundu wa Msimbazi haieleweki.

Zikiwa zimesalia raundi mbili ili Ligi Kuu Ghana kumalizika, Mukala anashika nafasi ya pili katika orodha ya wafungaji, akiwa amepachika mabao 14, nyuma ya Stephen Amankona wa Berekum Chelsea, aliyefunga magoli 15 mpaka sasa.

Taarifa zaidi zinasema Simba imetuma mawakala wake kwenda Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo (DRC), kwa ajili ya kusaka baadhi ya wachezaji wapya ambao watasaidia kuimarisha kikosi chao.

„Hivi sasa Simba hakuna masihara, kuna watu wamekwenda DRC, wengine Afrika Magharibi na wapo waliokwenda Ukanda wa Kusini zikijumuisha nchi za Angola, Botswana, Zambia kwa ajili ya kufanya skauti ya wachezaji bora," aliongeza mtoa taarifa wetu.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana, kwa sasa hawezi kusema lolote juu nani amesajiliwa hadi wakati mwafaka wa kufanya hivyo utakapofika.

Hata hivyo Ahmed aliweka wazi Simba imejiandaa kufanya usajili ‚mkubwa' ili kumaliza unyonge katika msimu ujao.

„Mashabiki wa Simba watulie, tunasajili na tukishamaliza tutawaambia, ila utakuwa usajili mkubwa sana ambao hawajawahi kuushuhudia katika misimu ya hivi karubuni," alionge-za.

Wakati huo huo, mlinzi wa kati ya timu hiyo, Kennedy Juma, huenda akajiunga na Coastal Union kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Chanzo chetu kingine kilisema Coastal Union imeshaanza mazungumzo na meneja wa beki huyo ili kupata saini yake na uamuzi huo umetokana na uzoefu alionao katika michuano ya kimataifa.

# MAJALIWA AKERWA GEITA GOLD FC KUSHUKA DARAJA

**Na Adam Fungamwango**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema moja ya sababu iliyopelekea Geita Gold FC kushuka daraja ni kutokana na mkoa wa Geita kushindwa kuzalisha na kuibua vipaji vipya vya wachezaji na kuongeza hali hiyo imemkera.

Geita Gold pamoja na Mtibwa Sugar zimeshuka daraja moja kwa moja na msimu ujao zitashiriki Ligi Kuu ya Championship wakati JKT Tanzania na Tabora United zinacheza mechi za mtoano ili kujinusuru na janga hilo.

**Akiwa ziarani Geita juzi, Majaliwa alisema hajafurahishwa na kiten do cha timu hiyo kushuka daraja na imetokana na wahusika hawakusima mia vizuri mchakato wa kuzalisha wachezaji wa ndani wa mkoa huo huku maeneo ya michezo yaki wa yamejaa nyasi.**

Majaliwa alisema mkoa umeshindwa kuimarisha miundombonu ya viwanja viwavyotumiwa kufanya mazoezi na vijana wapenda michezo na kutaja Uwanja wa Magufuli ulioko Chato, kwa sasa umetelekezwa bila kufanyiwa ukarabati.

"Timu imeshuka daraja, nataka niwaambie, hamkuimarisha, kuzalisha wachezaji ndani ya mkoa, na mmeshindwa kuzalisha kwa sababu hakuna maeneo mengi ya kuchezea vijana, na hata huu uliopo umejaa nyasi ndefu, ina maana vijana hamuutumii, na vijana mpo.

Leo Tanzania tunasajili wachezaji wengi sana kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, hivi nyinyi mmeshindwa kucheza? Yaani mpaka tunaagiza wadaka mpira (magolikipa), yaani vijana wetu wanashindwa kudaka mpira unaokuja kweli?" alihoji kiongozi huyo.

Majaliwa pia alimwagiza Ofisa Utamaduni kusimamia hilo, ili baadaye Geita Gold iwe timu imara na yenye wachezaji bora wanaotoka mkoani hapo.

Geita Gold, imeshuka daraja msimu huu, baada ya kumaliza nafasi ya 15 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kukusanya pointi 25 tu.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi ya kujenga utimamu wa mwili kabla ya kuanza safari ya kurejea Tanzania wakitokea Indonesia kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa: **PICHA: TFF**

# Lusajo amfunika Aziz Ki

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kaimu Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, akiteuliwa kuwa Kocha Bora wa Mei, straika wa Mashujaa FC ya Kigoma, Reliants Lusajo, ametwaa tuzo ya Mchezaji Bora akiwabwaga, Stephanie Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum ‚Fei Toto' kutoka Azam FC.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi jana imesema, Mgunda aliwashinda Miguel Gamondi wa Yanga na Bruno Ferry wa Azam FC.

Mgunda aliiongoza Simba kukusanya pointi 19 katika michezo saba iliyocheza, ikishinda sita na kutoa sare moja.

Iliifunga Tabora United na JKT Tanzania mabao 2-0, mabao 3-0 dhidi ya Azam FC, KMC na Dodoma Jiji bao 1-0, Geita Gold mabao 4-1, na sare ya bao 1-1 dhidi ya Kagera Sugar.

Lusajo, aliyesajiliwa na Mashujaa akitokea Namungo, aliwazidi Aziz Ki na Fei Toto, ambao waliingia katika hatua ya fainali ya kuwania tuzo ya mwezi huo huku akiifungia timu yake mabao matano na kuhusika kwenye ‚asisti' mbili kwenye mechi za hatua ya lala salama.

Tuzo za jumla zinazotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), zitafanyika mapema kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa mashindano.



# *Simba, Yanga kuanzia...*

INATOKA UK. 24

zoshiriki mashindano hayo Mfumo wa Mashindano wa shirikisho hilo (CMS).

Timu zitakazoshiriki mashindano hayo pia zitatakiwa kufuata kalenda ya usajili ambayo itaanza Julai Mosi hadi 20, mwaka huu kwa ajili ya wachezaji watakaocheza mechi za hatua ya awali wakati usajili utakaoanza Julai 21 hadi Agosti 31 utawahusu nyota watakaoshiriki mechi ya hatua ya pili.

Dirisha lingine la tatu litafunguliwa kuanzia Septemba Mosi hadi 30 na litawahusu wachezaji watakaoshiriki mechi za hatua ya makundi na timu zitakazosonga mbele katika michuano hiyo zitaruhusiwa kuongeza idadi ya wachezaji wasiozidi saba katika kipindi cha Januari Mosi hadi 31, mwakani.

Iliongeza hatua ya pili ya mashindano ya Kombe la Shirikisho imeondolewa wakati timu zitakazotolewa katika Ligi ya Mabingwa Afrika hazitahamia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho kama ilivyokuwa misimu iliyopita.

Hata hivyo kwa upande wa visiwani, bado haijajulikana itawakilishwa na timu zipi katika mashindano hayo ya CAF mpaka pale Ligi Kuu Zanzibar na mashindano ya Kombe la ZFF yatakapomalizika.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), limesema zimebaki raundi tatu ili kukamilisha kwa msimu wa 2023/2024.

# Michezo

Jumatano Juni 5, 2024
Nipashe



Rasmi Mbappé mali ya Madrid UK. 21



Beki wa Yanga, Dickson Job, akilibusu kombe la ubingwa wa mashindano ya FA baada ya timu yao kuibuka na ushindi wa penalti 6-5 dhidi ya Azam FC, baada ya kurejea Dar es Salaam wakitokea Zanzibar ilipofanyika fainali ya michuano hiyo ya mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# Simba SC, Yanga kuanzia ugenini CAF

## ●●● Dirisha la usajili la kimataifa kufunguliwa rasmi Julai Mosi...

**CAIRO,** Misri

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga pamoja na Simba wataanzia ugenini katika mashindano ya Kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika, watakayoshiriki katika msimu mpya wa michuano hiyo.

Timu nyingine za Tanzania Bara zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ni Azam FC ambayo itapambana katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Coastal Union iliyofuzu kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, Azam na Coastal Union, zenyewe zitaanza michuano hiyo kwenye hatua ya awali na mechi zao za kwanza zitachezwa nyumbani kati ya Agosti 16 na 18, mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa na CAF, inasema klabu hizo mbili kutoka Tanzania, Yanga na Simba zitaanza kuwania ubingwa wa mashindano kuanzia raundi ya pili na mechi zao za kwanza zitachezwa ugenini na kumalizia nyumbani.

CAF katika taarifa yake imesema pia hatua ya awali ya mashindano hayo ya ngazi ya klabu kwa msimu wa 2024/2025 itaanza rasmi kufanyika kati ya Agosti 16 na 18, mwaka huu.

Shirikisho hilo pia limesema mechi za hatua ya makundi zitafanyika kati ya Oktoba na Desemba, mwaka huu huku michezo ya mtoano ya mashindano yote ikitarajiwa kuchezwa kati ya Machi na Mei, mwakani.

CAF pia imethibitisha nchi 12 ambazo zina pointi nyingi katika viwango vya ubora vitatoa timu mbili katika kila mashindano (mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na mbili katika Kombe la Shirikisho Afrika), ni pamoja na Algeria, Angola, Ivory Coast, Misri, Libya, Morocco, Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Afrika Kusini, Sudan, Tunisia na Tanzania.

Wakati huo huo CAF pia imefungua ukurasa kwa nchi wanachama wake kuwasilisha majina ya timu zitaka-

INAENDELEA UK. 23

## Straika wa Uganda kutua Msimbazi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeanzisha mazungumzo na straika, Steven Mukwala wa Asante Kotoko ya Ghana kwa ajili ya kampeni yake ya kujiimarisha kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Habari kutoka ndani ya Simba zinasema mazungumzo na mchezaji huyo, raia wa Uganda yanakwenda vyema na anatarajia kutua nchini siku yoyote nchini baada ya kumaliza kuitumikia nchi yake (Uganda Cranes).

Chanzo hicho kilisema baada ya Mukwala kuichezea Uganda Cranes, straika huyo atasafiri moja kwa moja kuja Dar es Salaam ili kukamilisha mchakato na kusaini mkataba.

„Ninavyojua tayari mchezaji huyo ameshaondoka Ghana kwa ajili ya kujiunga na Uganda Cranes, wao watacheza na Botswana, kwenye Uwanja wa Mandela, baada ya hapo atakuja Dar ili kukamilisha mazungumzo na wakiafikiana atasaini mkataba," kilisema chanzo

INAENDELEA UK. 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >